SportPesa
TZS. 1,013,643,920
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**Mama** adaiwa kuchoma moto pua na mdomo wa mwanawe

UKURASA 4


Nipashe TESA
Jumanne Machi 8, 2022
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI

Mama msomi aliyepenyeza mabinti lukuki UDSM (Ukurasa 13)

Kinamama wa Zanzibar bega kwa bega uchumi buluu, bidhaa jongoo (Ukurasa 12)

KILELE SIKU YA WANAWAKE

**Asha- Rose Migiro**, hawezi kusahaulika kwenye orodha ya viongozi wa dunia, alikuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN) wa kwanza mwanamke na kutoka Afrika.

Ni 'Super Woman' wa Tanzania, Rais Samia Suluhu Hassan. Mama wa misingi ya haki, mtumishi wa wanyonge, mtetezi wa kila mmoja kwa usawa wa kijinsia...kazi inaendelea kwa kasi.

**Getrude Mongella**, anatisha kiuongozi, ameshika nyadhifa nyingi ni Rais wa kwanza wa Bunge la Umoja wa Afrika. Kuanzia 1993 hadi 1995, alikuwa Katibu Mkuu wa Mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Masuala ya Wanawake uliofanyika Beijing China mwaka 1995 kwa mafanikio.

Katibu Mkuu Kiongozi SMZ, **Zena Ahmed Said**, yuko makini na mahiri kuonyesha kuwa wanawake wanaweza.

Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, **Dk. Stergomena Tax**, ameandika historia SADC akiwa ni mwanamke wa kwanza kuwa Katibu Mkuu wa Jumuiya ya SADC.

**Nenelwa Mwihambi** ni Katibu wa Bunge wa kwanza mwanamama, amedhihirisha umahiri uongozi wa muhimili muhimu wa dola.

**Profesa Esther Mwaikambo** ni daktari wa kwanza mwanamama nchini, tena ni bingwa wa magonjwa ya watoto, anadhihirisha kuwa wanawake hawajawahi kushindwa sayansi.

UKURASA 11

Nipashe
Jumanne Machi 8, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580878
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US



Mama lishe Edina Michael akiwahudumia wateja huku akiwa na mtoto wake Daniel Robert (1) mgongoni kama alivyokutwa eneo la Soko la Nyerere Square jijini Dodoma jana. **PICHA:IBRAHIM JOSEPH**

SIKU YA WANAWAKE

# Wadau wapaza sauti kuhusu uongozi na ukatili kingono

UKURASA 2

## YALIYOMO

**UKURASA WA 4**
**PM AZINDUA MRADI WA BIL. 16/- WA MAZIWA**
WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amezindua mradi mkubwa wa Ushirikiano wa Wasindikaji...

**UKURASA WA 19**
**WAKILI AJIENGUA KESI YA KINA OLE SABAYA**
WAKILI Fridolin Bwemelo wa mshtakiwa wa tatu katika kesi ya uhujumu uchumi...

## Watanzania waeleza madhila waliyopitia kukimbia vita Ukraine

UKURASA 3



Rais Samia Suluhu Hassan akipokea vifaa vya kusaidia kusikia kwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna (kulia), kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum wa Shule ya Sekondari ya Benjamin Mkapa, Uhuru Mchanganyiko, Jangwani na Shule ya Msingi Uhuru Wasichana, katika hafla maalumu ya uboreshaji elimu kwa kuzingatia mahitaji maalum. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Walichoteta Rais Samia, mtoto mwenye ulemavu

UKURASA 2

**MICHEZO** **NABI ALIA MAJERUHI, AGEUKIA WAAMUZI** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akitabasamu wakati akishuhudia Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Kilimo Tanzania (TADB), Frank Nyabundege (chini kulia), akikabidhi mkataba wa makubaliano kwa mwakilishi wa Bill & Mellinda Gates Foundation, Marcela McClatchey (kushoto), taasisi hiyo ilitoa ruzuku ya shilingi bilioni 16 kwa TADB kwa ajili ya kusaidia sekta ya maziwa. Kulia kwa Waziri Mkuu ni Waziri wa Mifugo, Mashimba Ndaki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## SIKU YA WANAWAKE

# Wadau wapaza sauti, uongozi, ukatili kingono

**Na Waandishi Wetu**

WAKATI wanawake wakiadhimisha siku yao leo, wadau wamesema rushwa ya ngono ni tatizo linalotafuna ndani kwa ndani, huku wakitaka wanawake zaidi kuongoza katika sekta mbalimbali nchini.

Baadhi ya wadau hao ni Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA) na Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika, Tawi la Tanzania (MISA TAN).

Taarifa kwa vyombo vya habari iliyotolewa jana na TAMWA, ilisema kinaangalia usalama wa wanahabari wanawake katika vyumba vya habari nchini kutokana na kuwapo kwa mwendelezo wa matukio, ushahidi na ripoti za kitafiti zinazoonyesha kuwa wanahabari wanawake bado wanapitia unyanyasaji wa kingono katika vyumba hivyo.

Ilisema maadhimisho ya Siku ya Wanawake kwa mwaka huu, yamebebwa na kaulimbiu isemayo; "Kizazi cha Haki na Usawa kwa Maendeleo Endelevu". Kauli hii ni kutaka kuweka usawa katika vyumba vya habari baada ya kubaini kuna mdudu anayetafuna tasnia ya habari kimya kimya.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, utafiti uliofanywa na Asasi ya Wanawake katika Habari Afrika (WIN) ulibaini kuwa, asilimia 41 ya wanawake wanahabari waliwahi kufanyiwa unyanyasaji wa kingono wakiwa katika maeneo ya kazi.

Chama hicho kimesema wakati Siku ya Wanawake Duniani ikiadhimishwa, TAMWA inahimiza wamiliki wa vyombo vya habari, watunga sera, serikali na wanahabari wote kwa ujumla kutupia jicho unyanyasaji na ukatili wa kingono unaofanywa ndani ya vyumba vya habari.

"Unyanyasaji wa kingono kwa wanahabari iwe ndani au nje ya vyumba vya habari, una madhara makubwa katika chombo cha habari, taaluma ya habari, aina ya habari zitakazoandikwa na hata katika maendeleo ya nchi yenyewe," alisema Mkurugenzi Mtendaji wa TAMWA, Dk. Rose Reuben.

Alisema, udhalilishaji wa kingono kwa wanahabari wanawake, unachagiza wanahabari wengi wa kike kuikimbia tasnia na hilo limesababisha kupoteza vipaji lukuki ambavyo vingekuwa kama kusingekuwa na bughudha hiyo.

Alisema katika utafiti uliofanywa na TAMWA kwa kushirikiana na Mfuko wa Wanawake Tanzania (WFT) mwaka 2021, kuhusu hali ya rushwa ya ngono ndani ya vyumba vya habari, ilibainika kuwa wanahabari wanawake wamewahi kukutana na udhalilishaji huu, kimwili, kimaneno na hata baadhi walifukuzwa kazi.

Kwa upande wa Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika, Tawi la Tanzania (MISA-TAN), ilitoa wito kwa serikali, sekta binafsi na taasisi mbalimbali kuhakikisha wanawake wanapewa nafasi za uongozi kwenye taasisi hizo sawa na wanaume.

"MISA-Tanzania inaunga mkono kauli mbiu ya mwaka huu inayolenga kuvunja upendeleo wa jinsia, yaani #BreakTheBias, kwa kufanya kampeni maalumu kwenye mitandao ya kijamii kwa kuwatambua baadhi ya wanawake vinara kwenye sekta ya habari nchini," ilisema taarifa hiyo.

"Baadhi ya vyombo vingi vya habari nchini bado vina mfumo dume na wanawake hupata changamoto nyingi kufikia nafasi za juu za uongozi, wengi wameishia kukaimu, wasaidizi na kazi za kawaida licha ya kuwa na uwezo wa kitaaluma na uzoefu wa majukumu husika," alisema Salome Kitomari, Mwenyekiti wa MISA-Tanzania.

"Vyombo vingi vya habari ukiingia unaona ni duniani ya wanaume 'mens world'. Kinachokosekana ni kuwaamini na kuwaacha watekeleza majukumu hayo licha ya sifa na vigezo vinavyotakiwa, ndiyo maana kwenye vyuo vya uandishi wa habari wanahitimu wanawake wengi, wanaingia kwenye vyombo vya habari wengi hubaki kuwa ripota na inapotokea nafasi ya uongozi hawapewi siyo kwasababu ya uwezo ni kwa sababu ya mfumo, wengine hukata tamaa na kwenda kufanyakazi nyingine," aliongeza.

"MISA-Tanzania inatoa wito kwa vyombo vya habari na taasisi mbalimbali za tasnia hii, kuwa na sera mahsusi zinazotekelezeka zenye lengo la kuondoa mfumo dume huo kwenye taasisi zao kwa kuhakikisha kuwa wanawake wanajengewa uwezo, wanaaminiwa na kupewa nafasi za uongozi kwa mujibu wa sifa na vigezo."

Taarifa hiyo ilisema utafiti uliofanywa mwaka 2019 na Baraza la Habari Tanzania (MCT), ulibaini kuwa wanawake wanapewa nafasi za kati na za chini kwenye vyombo vya habari vingi nchini na huwa ni ngumu kwao kushika nafasi za juu za uongozi hata kama wana uzoefu au elimu zaidi kuliko wanaume.

Utafiti huo uliopewa jina la "Challenging the Glass Ceiling: Study of Women in the Newsroom in Tanzania", ulibaini pia kuwa waandishi wa habari nchini hupangiwa kuripoti matukio ambayo siyo makubwa au mazito, ambayo mara nyingi hupangiwa waandishi wa habari wanaume.

Ilisema watafiti waliongeza kuwa kuna idadi ndogo ya waandishi wa habari wanawake kwenye vyombo vya habari, licha ya kuwa wanawake wengi huhitimu vyuo vya uandishi wa habari nchini kuliko wanaume.

## Walichoteta Rais Samia, mtoto mwenye ulemavu

**Na Maulid Mmbaga**

RAIS Samia Suluhu Hassan ameeleza alichozungumza faragha na mwanafunzi Emanuel Mzena, akiahidi kutimiza ndoto zake, ikiwamo kumsomesha nje ya nchi na kumfungulia taasisi kwa ajili ya kuwasemea watoto wenye mahitaji maalumu.

Akihutubia wanafunzi wa Shule ya Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam jana, Rais Samia alisema mwanafunzi huyo ameishukuru serikali na mama yake kwa jitihada alizozifanya kuhakikisha anasoma.

"Aliniambia 'mama nashukuru sana serikali, namshukuru sana mama angu, akamwita malikia wa nguvu, kwamba pamoja na changamoto alizonazo za maisha, amejitahidi nimesoma mpaka kufikia mahala nilipo, nitafanya mwaka huu mtihani wa kidato cha sita.

"Akaniambia 'sina matumaini ya kupata ajira za serikali kwa hivi nilivyo, lakini nakuomba mama nikimaliza kidato cha sita nisomeshe nje'.

"Na la pili nifungulie taasisi yangu mwenyewe maalumu, lengo langu ni kuwasemea watoto kama mimi waliofichwa majumbani, watolewe waje wapate elimu shuleni'. Hilo ndilo nililoongea na Emanuel tukiwa peke yetu pamoja na mengine mawili matatu ambayo ni siri, lakini hilo nimeona niwaibie na mimi nimeahidi nitafanya hivyo," Rais Samia alisema.

Rais pia aliwapongeza walimu kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kutoa elimu na kuwalea watoto katika maadili mema, huku akiwatoa shaka wanafunzi, walimu na walezi kuwa serikali inatambua vikwazo vinavyowakabili watoto wenye mahitaji maalumu nchini.

Alisema serikali inafanya jitihada kuhakikisha inaweka mazingira rafiki ya kufundishia na kujifunzia ili kila Mtanzania anufaike na fursa ya elimu kwa manufaa binafsi na taifa kwa ujumla.

Rais alisema serikali imeendelea na mkakati wa kitaifa wa elimu jumuishi ambao utazingatia utoaji wa elimu jumuishi katika ngazi zote za elimu ikiwamo ya awali, msingi, sekondari, ualimu, vyuo vya ufundi, maendeleo ya jamii, elimu ya watu wazima na ya juu ili kutoa elimu bora kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

"Tunafanya hivyo kwa sababu tunatekeleza azimio la kimataifa. Azimio Na. 4 katika maazimio ya maendeleo endelevu linazungumzia elimu limetutaka tutoe elimu kwa wote, watoto wa kike na wa kiume, isiyolipiwa, yenye hadhi na watoto wote wawe na usawa katika kupata elimu," alikumbusha.

Rais Samia alisema serikali imeandaa miongozo kwa ajili ya kurahisisha utoaji wa elimu maalumu na jumuishi nchini, ikiwamo usimamizi wa uendeshaji wa taasisi zinazotoa elimu maalumu na jumuishi kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu wa mwaka 2020/21.

Pia mwongozo wa ujenzi wa majengo ya serikali yanayozingatia wanafunzi wenye mahitaji maalumu na mwongozo wa lishe shuleni wa mwaka 2021, akiwahakikishia Watanzania kwamba mawaziri husika wanaifanyia kazi miongozo hiyo.

Rais Samia alisema kuwa ili kuhakikisha watoto wote wenye mahitaji maalumu wanapata fursa ya elimu, mwaka 2021 serikali ilifanya ubainishaji wa watoto hao ambao wamefikisha umri wa kuanza shule.

Alibainisha kuwa katika kata 3,785, sawa na asilimia 95.7 ya kata zote nchini (3,956), uainishaji ulibaini watoto 28,968 wenye mahitaji maalumu kati ya 59,784 walichunguzwa.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, alisema kwa kipindi cha mwaka mmoja wizara ilipatiwa Sh. bilioni 101.9 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa, matundu ya vyoo, mabweni, maabara, nyumba za walimu, mabwalo pamoja na miundombinu mbalimbali katika shule za msingi na sekondari.

Mkuu wa Shule hiyo, Joseph Deo, alisema ina wanafunzi wenye mahitaji maalumu 109 (wavulana 52 na wasichana 57) na kikwazo kikuu kwao ni ukosefu wa chumba cha kupimia wanafunzi wenye tatizo la kusikia, vifaa vyake na viti mwendo kwa ajili ya wanafunzi wenye ulemavu wa miguu. Rais aliahidi kutatua vikwazo hivyo.

## HABARI KITAIFA



Maelfu ya raia kutoka nchini Ukraine wakisubiri treni kituo cha Zahony, kuelekea Budapest, Hungary, jana. **PICHA: AP**

# Watanzania waeleza madhila wanayopitia kukimbia vita Ukraine

**Na Christina Mwakangale**

WANAFUNZI wa Kitanzania walioko nchini Ukraine kwa ajili ya masomo, ambao baadhi wamefanikiwa kuondoka nchini humo, wameelezea namna walivyokutana na madhila tofauti wakitumia njia tofauti, ikiwamo usafiri wa kukodi, kufika nchi jirani na kupata hifadhi kwa gharama ya takribani Dola za Marekani 500 hadi 800.

Mmoja wa wanafunzi hao akizungumza na DW Redio, jana, na kujitambulisha kwa jina la Msabaha Salum Msabaha, ambaye anasoma katika Chuo Kikuu Sumy, kilichoko Mashariki mwa Ukraine, anasema imewapasa kutumia usafiri wa kukodi hadi nchini Hungary, kwa gharama ya Dola 400.

Anasema yeye pamoja na wenzake kutoka Tanzania, walifanikiwa kuingia Hungary, kwa kutumia siku kadhaa na kuwapasa kila mmoja kutumia nauli inayofikia Dola 400 hadi 800 kufika umbali wa kilomita zisizozidi 180.

"Tupo Hungary hapa Watanzania kadhaa, usafiri ni mgumu na si wote ambao mtapata, unabahatisha hamuwezi kupata wote. Na ni ghali kwa sababu madereva wana 'take-risk' kutokana na hali yenyewe.

"Si kila mtu anaweza akafanya maamuzi kwa hiyo wachache tulifanya maamuzi na kubahatika kupata gari kutoka Sumy hadi nje ya mji, vikwazo ni vingi. Kutoka Sumy kiwango cha chini ni Dola 400 unalipia kwa mtu mmoja, ila wapo waliolipia hadi Dola 800, watu wanne tu kwa gari ndogo," alisema Msabaha.

"Mnaachwa eneo ambako mtasubiri usafiri wa treni ambao pia sio wote mtapata, unaweza ukapata au usipate, ukitoka kwenye treni sasa kwenda mipaka tofauti, iwe Hungary, Poland, nako huko ujipange kwa kutumia dola nyingine tena Dola 100 au 80," anasema Msabaha.

Anasema kwamba licha ya kuwapo mapigano kila siku maeneo tofauti waliamua kusafiri kama wakimbizi na mara ya kufika maeneo ya ukaguzi walitakiwa kuonyesha pasi za kusafiria.

"Kuna check point nyingi (vituo vya ukaguzi) sijakutana na watu wowote wa kunipokea zaidi ya Watanzania waishio hapa (Hungary) wamejitolea kuweka mawasiliano yao, wametupokea vizuri tupo salama kwa sasa.

"Kuna free au fair accommodation kwa siku 42 unaweza ukapata ila inategemeana na ratiba zako au unaweza ukatafuta eneo lingine ukawa salama zaidi. Ila mimi binafsi sijapigiwa simu ya kutueleza namna ya kutusaidia."

Mwanafunzi mwingine anayesoma chuo hicho, akitokea Tanzania, ambaye alijitambulisha kwa jina moja la Ellen, anasema kwamba hofu ipo kwa takribani wanafunzi wote na kusali kwenye hosteli.

"Kuna maeneo hakuna maji, chakula, umeme na hamjui hatima yenu kwa kweli inasikitisha. Huwa tunaenda kwenye maduka ya dawa tunakuta hamna, tunahitaji msaada wa haraka na ule wa kiutu, tumechoka tunaomba msaada. Baridi ni kali sana halafu hakuna chakula, tumeathirika kisaikolojia," anasema Ellen akizungumza na kituo cha televisheni Aljazeera.

"Nimezungumza na wazazi wangu walioko Tanzania, lakini nazungumza nao bila kuwapa hofu ila hali si nzuri, kwa siku 11 tunahitaji msaada, wanafunzi tunapata shida hata ukiangalia kwenye vyombo vya habari utabaini ninachokisema. Kuna milio inaendelea kila mahali, kuna wanafunzi ambao ni wasichana wadogo kuliko mimi wanalia tu."

## NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kampuni ya **MBUZAX AUCTION MART AND COMPANY LIMITED, BROVITAS COMPANY LIMITED, JADA INVESTMENT LTD AND MOPEH COMPANY LIMITED** Kwa idhini tuliyopewa na **FINCA MICROFINANCE BANK LTD** tunatoa muda wa siku 14 kwa wadaiwa walioorodheshwa kwenye jedwali hapo chini wawe wamelipa madeni wanayodaiwa na **FINCA MICROFINANCE BANK LTD.** Kinyume na hapo tutalazimika kuuza kwa njia ya mnada wa hadhara mali walizoweka kama dhamana ya mkopo. Tarehe za kufanya minada zitatolewa kwa njia ya vipeperushi na magari ya matangazo kwenye sehemu dhamana zilipo.

| | NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA | | |
|---|---|---|---|
| | MBUXAZ AUCTION MART AND COMPANY LIMITED | | |
| S/N | JINA LA MDAIWA | AINA YA DHAMANA | MAHALI ILIPO DHAMANA |
| 1 | PENDO.S. NYENZE | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | ZINGA-BAGAMOYO-PWANI |
| 2 | ABDUL SALEH ABDALLA | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | MBWENI ZAHANATI-DAR ES SALAAM |
| 3 | MATEI M. MKUMBA | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | GOBA MATOSA-DAR ES SALAAM |
| 4 | ANDREW HAMSON KISANGA | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO | NYAKASAGWE- DAR ES -SALAAM |
| 5 | ADAM O. TENGEMU | NYUMBA YENYE MKAABA WA MAUZIANO | BOKO-DAR ES SALAAM |
| 6 | AMANI ABDUEL MSUYA | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | BOKO, CHAMA-DAR ES SALAAM |
| 7 | ANNA B. MOSHA | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | BUNJU - DAR ES SALAAM |
| 8 | NEEMA C. MBALAFU | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | KIMARA BARUTI-DAR ES SALAAM |
| 9 | JOSEPH BINA KISIWANI | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO | KIMARA GOLANI-DAR ES SALAAM |
| 10 | DISMAS REGINALIDI RUPIA | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | KILIMAHEWA-WAZO-HILI-DAR ES SALAAM |
| 11 | REVOCATUS EVARIST MADABA | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | KIPUNGUNI-DAR ES SALAAM |
| 12 | REHEMA J. MAKAME/ HAMISI JUMA MTABAZI | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO MALI YA HAMIS JUMA MTABAZI | TEGETA KWA NDEVU-DAR ES SALAAM |
| 13 | VITUS L. ANTONY | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO | GOBA - DAR ES SALAAM |
| | BROVITAS COMPANY LIMITED | | |
| 14 | THOMAS M MAYALLA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI ILIYOPO KWENYE KIWANJA NA. 149 KITALU E, MAJENGO KAHAMA | MAJENGO - KAHAMA |
| 15 | KHAMISI A. ASSAD | NYUMBA YENYE HATI MILIKI OLIYOPO KWENYE KIWANJA NA. 13 KITALU A, ISAKA KAHAMA | ISAKA - KAHAMA |
| 16 | G0DWIN G. MBISE | GARI AINA YA SUZUKI CARRY YENYE USAJILI NAMBA T477 CTX CHASSIS NA. DA52T259513 | ISAKA- KAHAMA |
| 17 | HANIFA E. MBUBU | KIWANJA CHENYE HATI YA MAUZIANO MALI YA EUNICE ALSON MGHAMBA | MHUNGULA- KAHAMA |
| 18 | RUKIA N. MOHAMMED | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO | ISAKA- KAHAMA |
| 19 | KULWA M. JEREMIAH | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO | SHUNU-KAHAMA |
| 20 | ROBERT M. GUMALI | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO | MBULU-KAHAMA |
| | MOPEH COMPANY LIMITED | | |
| 21 | FREDY MALI KAZI | NYUMBA YENYE HATI MILIKI ILIYOPO KIWANJA NA. 614, KITALU AH. | MHOGOLO-KAHAMA |
| 22 | THOMAS E SHAYO | NYUMBA YENYE HATI MILIKI KIWANJA NA.88, KITALU EE, SOKOLA MAJENGO | SOKOLA - KAHAMA |
| 23 | APOLINARY A MUTA | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO | MWIME - KAHAMA |
| 24 | JUMA DAUDI SAGUDA | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | NYANSHIMBI-KAHAMA |
| 25 | ASUMINI H NTILINGANIZA | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO | MASUMBWE-KAHAMA |
| | JADA INVESTMENT LTD | | |
| 26 | MAFUBILLO GENERAL SUPPLIERS LTD | GARI AINA YA SCANIA (Model 113-320) YENEYE NAMBA ZA USAJILI T 769 BTV MALI YA ABDALLAH MASOUD NGOZI | DAR ES SALAAM |
| 27 | SAIDI ALLY SAID | GARI AINA YA NISSAN CIVILIAN YENYE NAMBA ZA USAJILI T355 DGE | DAR ES SALAAM |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
3. Mnunuzi atayeshinda anapaswa kulipa 25% ya bei aliyofikiwa siku ya mnada, na 75% iliyosalia atalipa ndani ya siku kumi na nne (14) toka tarehe ya mnada, Kinyume na hapo kiasi kilichotolewa awali hakitarudishwa na mnada utarudiwa tena.
4. Gharama zozote ikiwemo kubadilisha Hati miliki (transfer of ownership), na kumtoa mtu kwenye nyumba/eneo lililouzwa ni la mnunuzi.
5. Mnada utafanyika mahali ambapo dhamana zilipo na si vinginevyo.

**KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA NAMBA**

**Mkurugenzi Mtendaji**
**Mbuzax Auction Mart and Company Limited**
**S.L.P 62070 Dar es Salaam**
**Simu: 0755 506970/0716763571**
**NA**
**Mkurugenzi Mtendaji.**
**Mopeh Company Limited**
**S.L.P 590**
**Dar es Salaam**
**Simu: 067335528**
**NA**
**Mkurugenzi Mtendaji,**
**Brovitas Company Limited**
**S.L.P 1305**
**Songea**
**Simu: 0628555260**

**Na**
**Mkurugenzi Mtendaji,**
**Jada investment Limited,**
**P.O. Box 69098**
**Dar es Salaam**
**Simu: 0788498699**
**NA**
**Finca Microfinance Bank Ltd**
**P.O. Box 78783**
**Simu: 0768790399, 0754774949**

216735002

# Mama adaiwa kumchoma moto mwanawe mdomo, pua

Na Godfrey Mushi, MOSHI

MKAZI wa Newland Kijiji cha Mvuleni, Wilaya ya Moshi mkoani Kilimanjaro, Grace Pima, anadaiwa kumchoma moto mtoto wake wa miaka mitano mdomo pamoja na pua.

Mama huyo anadaiwa kutekeleza kitendo hicho kwa kutumia banio linalotumiwa kuunganisha njia ya reli, pia inadaiwa alimfungia ndani mtoto huyo ambaye ni wa kiume (jina limehifadhiwa) kwa takribani saa 48.

Ukatili huo ulifichuliwa jana na Mjumbe wa Kamati ya Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA), Agness Moshi, wakati wa kikao kazi cha Mradi wa Paza Sauti, Tokomeza Ukatili, unaoendeshwa na Shirika la TUSONGE CDO.

Agness alisema mama huyo baada ya kutekeleza ukatili huo, anadaiwa kumfICHA ndani mtoto huyo na kuanza kumtibu majeraha kwa dawa za kienyeji, akiwa amemsiliba mdomoni na puani, majani mabichi yaliyotafunwa yanayodaiwa kuwa ni dawa.

"Tulipomkamata na kumuuliza kwa nini amemchoma mtoto wake, alituambia kwamba mtoto alitoa tusi. Nikamuuliza ni tusi gani hajielezi kitu kinachoeleweka.

"Huyu mama alifanya ukatili huo Februari 28, usiku na sisi tulipata taarifa kutoka kwa majirani zake Machi 2, mwaka huu, baada ya kumfungia ndani kwa saa 48 akimtibu kwa dawa za kienyeji za mitishamba ili asibainike.

Alisema baada ya kupata taarifa hiyo walimchukua mama na mtoto na kuwapeleka Ofisi ya Mtendaji wa Kijiji cha Mvuleni.

Agness alisema baadaye waliondoka na mtoto kwenda Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Kilimanjaro ya Mawenzi ili akapatiwe matibabu.

Alieleza kwamba mama anayedaiwa kutekeleza kitendo hicho walimpeleka Dawati la Jinsia la Polisi, Wilaya ya Moshi na walipewa fomu namba tatu kwenda Mawenzi.

Alieleza kuwa hivi sasa mama huyo anashikiliwa kituo cha polisi, kwamba anaendelea kuhojiwa.

Ofisa Ustawi wa Jamii wa Wilaya ya Moshi, Habiba Bhou, alisema: "Sisi tunatoa wito kwa jamii kuacha kujichukulia sheria mkononi, kwa sababu ukisoma kwenye elimu ya malezi na makuzi, hilo tukio la mama kumchoma mtoto wake mdomo na pua ili asimtukane, iko namna.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Mvuleni, Kata ya Mabogini, Veronica Mjinja, alisema mama huyo alikamatwa na wananchi wapatao 15 wenye hasira, ambao baada ya tukio hilo walitaka kumdhuru.

Ofisa wa Polisi Kata ya Mabogini, Mkaguzi Msaidizi, Japhary Kalinga, alisema kila mzazi au mlezi anatakiwa kujua kwamba mtoto yeyote mwenye umri chini ya miaka tisa, hata akifanya jambo baya, sheria haimhusishi na makosa ya jinai.




Mkurugenzi wa Mawasiliano, Beatrice Singano, akiongea na waandishi wa habari wakati akitangaza habari njema kwa wateja wake wote nchini wanaotumia huduma za vifurushi vya muda wa maongezi (bando za muda wa maongezi) kwa kuongeza dakika za bando kwa zaidi ya mara 2 pamoja na muda wake wa kutumika gharama ikiwa ni ileile. Kushoto ni Meneja Uhusiano Airtel, Jackson Mmbando. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## MWAKA MMOJA SAMIA IKULU

# Uhaba wa sukari kuwa historia nchini

Na Mwandishi Wetu

SERIKALI imesema uhaba wa sukari utakuwa historia nchini kutokana na uwekezaji mkubwa unaoendelea kwenye uzalishaji wa bidhaa hiyo.

Uwekezaji huo unajumuisha upanuzi wa Kiwanda cha Sukari Kilombero mkoani Morogoro kutoka kuzalisha tani 110,000 kwa sasa hadi tani 250,000 kwa mwaka.

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alibainisha hayo jana jijini Dar es Salaam, alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio yao katika mwaka mmoja wa Rais Samia Suluhu Hassan madarakani.

Alisema upanuzi unaoendelea wa Kiwanda cha Sukari Kilombero utagharimu Sh. bilioni 540, pia akibainisha uwekezaji katika viwanda vya sukari unaoendelea katika mikoa ya Mtwara, Pwani, Iringa na Morogoro.

Bashe alisema kuwa kufikia mwaka 2025, ambao ni ukomo wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Juni 1999-2025), hakutakuwa na uhaba wa sukari tena nchini na Tanzania itakuwa miongoni mwa nchi zinazozalisha sukari nyingi kwa ajili ya mauzo ya nje.

Takwimu rasmi za serikali zinaonyesha kwa mwaka mahitaji ya sukari nchini yanakadiriwa kuwa tani 710,000. Kati yake, tani 545,000 ni kwa matumizi ya kawaida ya nyumbani na tani 165,000 ni kwa mahitaji ya viwandani.

Kwa mujibu wa Bodi ya Sukari, uzalishaji wa sukari kwa sasa nchini ni tani 370,000 kwa mwaka.

Alipoulizwa kuhusu hatua zilizochukuliwa na wizara kuwasaidia wakulima wa miwa mkoani Morogoro waliopata hasara kutokana na kutoanza kwa Kiwanda cha Sukari Mkulazi, Bashe alisema miwa yao ilipelekwa Kiwanda cha Sukari Mtibwa na serikali imekubaliana na Benki ya Azania kuwasaidia wakulima hao.

**MAFANIKIO**

Waziri huyo alisema kuwa kwa mwaka mmoja mafanikio yao yanajumuisha serikali kuzipatia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya (NFRA) na Bodi ya Mazao Mchanganyiko (CPB) jumla ya Sh. bilioni 129 kwa ajili ya ununuzi wa mazao ya nafaka ambayo yatauzwa katika masoko ya ndani na nje ya nchi.

Alisema serikali pia imeongeza bajeti ya utafiti kutoka Sh. bilioni 7.35 hadi Sh. bilioni 11.63, huduma za ugani kutoka Sh. milioni 603 hadi Sh. bilioni 11.5, umwagiliaji Sh. bilioni 17.7 hadi Sh. bilioni 51.48, uzalishaji wa mbegu kutoka Sh. bilioni 5.42 hadi Sh. bilioni 10.58.

Alisema wizara pia imefanikiwa kufungua masoko mapya ya mazao nje ya nchi ikiwamo soko la parachichi (India na Afrika Kusini) na ndizi (Kenya) baada ya kukidhi viwango vya ubora.

Bsshe alisema CPB pia imefungua vituo vya mauzo katika miji ya Juba (Sudan Kusini) na Lubumbashi (DR Congo) na kukodi maghala yenye uwezo wa kuhifadhi tani 5,000 na 2,000 mtawalia.

"NFRA wamenunua tani 110,516.717 za mahindi na hivyo kuwa na akiba ya tani 214,000 za nafaka katika maghala yake. Tumefanikisha uuzaji wa soya nje ya nchi kufikia tani 53,594.35 mwaka 2020/21 kulinganishwa na tani 2,647 mwaka 2019/2020. Kampuni 80 za Kitanzania zimesajiliwa kuuza soya nchini China.

## PM azindua mradi wa bil. 16/- usindikaji maziwa

Na Mwandishi Wetu

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amezindua mradi mkubwa wa Ushirikiano wa Wasindikaji na Wazalishaji katika Tasnia ya Maziwa Tanzania (TI3P).

Mradi wa TI3P ni wazo mama la serikali kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) kwa kushirikiana na taasisi ya Bill & Melinda Gates Foundation na unalenga kuondoa changamoto iliyopo katika sekta ya mifugo na maziwa nchini, ukilenga kuwafikia wafugaji 100,000 na viwanda kati ya tisa na 12.

Taasisi ya Bill & Mellinda Gates Foundation ya nchini Marekani, imetoa ruzuku ya Dola za Kimarekani milioni saba (Sh. bilioni 16.2).

Waziri Mkuu alisema mradi huo utaongeza tija katika uzalishaji wa maziwa, ukusanyaji wa maziwa katika mfumo ulio rasmi, kukuza uwezo wa viwanda katika uchakataji wa maziwa na kupanua wigo wa soko la bidhaa za maziwa.

"Tanzania imeendelea kuwa muagizaji mkubwa wa maziwa kutoka nje ya nchi, huku zikitumika angalau shilingi bilioni 15 kwa mwaka. Kiwango hiki cha fedha ni kikubwa ikilinganishwa na fursa iliyopo katika sekta ya maziwa nchini," alisema Majaliwa.

Alisema licha ya Tanzania kushika nafasi ya pili kwa idadi ya mifugo barani Afrika, sekta ya mifugo inachagia asilimia 7.4 pekee kwenye Pato la Taifa. Kwa sasa, sekta ndogo ya maziwa inachangia asilimia 2.3 ya pato la taifa, na inakua kwa wastani wa asilimia tano pekee kwa mwaka.

Pia, uzalishaji wa maziwa umeongezeka kwa kiwango kidogo kutoka lita bilioni 2.1 mwaka 2016, hadi kufikia lita bilino 3.1 mwaka 2021. Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji TADB, Frank Nyabundege, alisema "Mradi huu wa TI3P ambao tunaingia katika makubaliano leo na taasisi ya Bill and Melinda Gates Foundation, unalenga kupandisha mchango wa sekta ya maziwa kwenye pato la kupitia uhamasishaji wa uwekezaji kutoka sekta ya umma na sekta binafsi ili kuongeza pato la taifa kwa maendeleo ya taifa letu."

Kwa mujibu wa Mkurugenzi huyo, serikali imekubali kufanikisha kiasi cha Dola za Marekani milioni 40 kwa ajili ya kuongeza nguvu ya uwekezaji katika mradi huo, huku taasisi ya Bill and Melinda Gates Foundation ikitoa msaada wa kiasi cha Dola milioni saba.

"Tayari fedha hizo zimeshafika nchini kwa ajili ya kuanza rasmi kazi ya kuleta mageuzi kwa wasindikaji na wazalishaji katika tasnia ya maziwa nchini," alisema Nyabundege.

Alibainisha kuanzia mwaka 2018 hadi Februari 28, 2022, TADB katika sekta ya maziwa pekee imewekeza Sh. bilioni 16.4 na kiasi cha Sh. bilioni 15.6 kimekopeshwa moja kwa moja kwa wafugaji na viwanda vya maziwa katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Iringa, Mara, Njombe, Tanga na Shinyanga.

Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Adam Malima, alisema mradi huo utasaidia kuongeza uzalishaji na tija kwa sekta ndogo ya maziwa katika mkoa wake ikiwa ni pamoja na kuboresha hali ya kiuchumi kwa wafugaji na mkoa kwa ujumla.

## TANGAZO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA SONGEA**

# TANGAZO LA ZABUNI

## NAMBA YA ZABUNI: LGA/102/2022/2023/NCS/01

## Ukusanyaji wa ushuru wa mazao ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Songea kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

# MWALIKO WA ZABUNI

Tarehe: 04/03/2022

Halmashauri ya Wilaya ya Songea imekasimia kukusanya mapato kutoka vyanzo mbalimbali.Miongoni mwa vyanzo hivyo ni ushuru wa mazao yote yanayosafirishwa kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Songea kuelekea sehemu mbalimbali za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

1. Halmashauri ya Wilaya ya Songea inapenda kuwaalika watu Binafsi , Makampuni , Ushirika, Taasisi au Vikundi vya watu vilivyosajiliwa kisheria, wenye nia na uwezo wa kufanya kazi ya kukusanya ushuru wa mazao kutuma maombi ya zabuni hii.
2. Mchakato wa Zabuni hii utafanyika kwa njia ya Ushindani wa Kitaifa kwa mujibu wa Kanuni za ununuzi wa umma za mwaka 2013 GN.446 pamoja na marekebisho ya Kanuni ya mwaka 2016 na ni wa wazi kwa Wazabuni wote kama ilivyoainishwa kwenye Kanuni.
3. Wazabuni wote wenye nia na sifa za kuomba Zabuni hii wanaweza kupata maelezo ya ziada na kukagua nyaraka za Zabuni kwenye ofisi ya Katibu wa Bodi ya Zabuni wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea, S.L.P 995, Songea kuanzia saa 01.30 Asubuhi hadi saa 9.30 Alasiri Siku za kazi.
4. Nyaraka za Zabuni zimeandaliwa kwa Lugha ya Kiswahili na zinauzwa TZS.100, 000/=. Malipo kwa ajili ya kununua Nyaraka za Zabuni yatafanyika baada ya kupewa Namba ya Malipo (Control Number) kupitia Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea, S.LP 995, Songea.
5. Muombaji ajaze Nyaraka za Zabuni kwa umakini na awasilishe Nyaraka halisi na nakala mbili( Original+ 2 copies) kwenye bahasha zilizofungwa vizuri juu ya bahasha aandike ‘’Uwakala wa kukusanya Ushuru wa mazao ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Songea , LGA/102/2022/2023/NCS/01 kisha zitumwe kwa Katibu wa Bodi ya Zabuni,Halmashauri ya Wilaya ya Songea,S.L.P 995, Songea kabla au tarehe 17.03.2022, Saa 4.00 Asubuhi, Siku ya Alhamisi.Ufunguzi wa Zabuni utafanyika siku ya Mwisho ya kuwasilisha Nyaraka za Zabuni kwa uwazi na mbele ya Wazabuni au Wawakilishi watakaohudhuria kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Halmashauri.
6. Zabuni zitakazo chelewa kufika kwa muda uliopangwa, sehemu ya Zabuni zitakazo tumwa kwa njia ya Kieletroniki mfano Fax,Email nk, Zabuni ambazo hazikufunguliwa siku ya ufunguzi na Zabuni ambazo hazikupokelewa hazitakubaliwa kufanyiwa tathmini bila kujali mazingira yoyote.
7. Waombaji wa Zabuni hii wanashauriwa kufanya utafiti ili waweze kuomba kazi kwa kiasi ambacho wataweza kukusanya na ambacho kipo ndani ya Makisio ya Halmashauri.
8. Halmashauri ya Wilaya ya Songea haitalazimika kisheria kutoa tuzo ya Zabuni kwa Muombaji aliyejaza makisio makubwa ambayo hayana uhalisia ukilinganisha na Makisio ya Halmashauri.
9. Muombaji anatakiwa kujaza kiasi ambacho ataweza kukusanya kitakachopatikana kwenye ushuru wa mazao kwa kila mwezi na kwa miezi yote kumi na mbili (12) kuanzia tarehe 01.07.2022 mpaka tarehe 30.06.2023.
10. Mapato yote yatakayotokana na mauzo ya mazao kupitia mfumo wa Stakabadhi Ghalani pamoja na Mamlaka ya Hifadhi ya Chakula ya Taifa (NFRA) hayatakuwa sehemu ya Zabuni, Halmashauri itahusika yenyewe katika kuyakusanya.

**Lucy S.Mbolu**

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA SONGEA**

216734902

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Usawa wa kijinsia muhimu kwa maendeleo endelevu

**LEO** ni Siku ya Wanawake Duniani ambayo kila nchi inasherehekea kwa utaratibu iliyojiwekea, huku lengo la msingi, likiwa ni ukombozi dhidi ya mwanamke ambaye ameachwa nyuma kwa miaka mingi kutokana na sababu za mfumo dume ambao ulitoa upendeleo kwa wanaume zaidi.

Kutokana na hali hiyo, wanawake walikosa fursa ya elimu, kumiliki mali, kuwa na maamuzi au kushika nafasi za maamuzi, kisiasa hadi kuwa wakuu wa nchi na nafasi nyingine muhimu kwenye jamii.

Siku hii hutumika kutambua, kuthamini na kuenzi mchango wa mwanamke kwa maendeleo ya jamii yake, nchi na dunia kwa ujumla, pia kupaza sauti juu ya changamoto za maeneo yenye kuhitaji marekebisho ili kufikia usawa usio na kikwazo kwa sababu ya jinsia.

Baadhi ya mila na tamaduni zimetumika vibaya kumkandamiza mwanamke kwamba anastahili kuolewa, kumburudisha mume, haruhusiwi kumiliki ardhi au kusema jambo na kusikilizwa. Kutokana na hali hiyo wengi hawakusoma hali iliyosababisha kuwa na wanaume wengi kwenye uongozi kuliko wanawake.

Kauli mbiu ya mwaka huu inalenga kuvunja upendeleo, kwa ajili ya kutoa usawa kwa jinsia zote kushiriki mchakato wa maendeleo na kufurahia maisha kama wengine, pasipo kukandamizwa.

Kwa sasa kuna mabadiliko makubwa kuanzia ngazi ya familia ambazo zimeona umuhimu wa elimu kwa mtoto wa kike na kuondoa dhana ya kuwa ataolewa hana msaada kwa jamii yake, wapo walioonyesha mfano licha ya kuolewa waliendelea kuzisaidia familia zao na ambao hawakuolewa vile vile wanabeba majukumu ya kutunza wazazi.

Sera na sheria mbalimbali zimetoa haki kwa mwanamke kumiliki ardhi na mali nyingine, lakini bado kuna changamoto kwenye utekelezaji, jamii kutambua na kuchukua hatua.

Kunapokosekana sera ya jinsia eneo la kazi ni rahisi kukuta jinsia moja ndiyo imepewa nafasi za juu, huku wengine wakiachwa katika kuweka usawa ni lazima kuhakikisha wote wanashiriki kwenye ujenzi wa nchi kwa maendeleo endelevu.

Wapo wanaofikiri kuwapa nafasi wanawake ni kuruhusu wanaume wakandamizwe au waonewe, wengine wameenda mbali kuwa wanawake wakishakuwa na nguvu ya kiuchumi wanaacha kuwa watii kwa waume au wakubwa zao, jambo ambalo kimsingi siyo kweli bali hutumika kama mbinu ya kumpunguzia nguvu mwanamke.

Nchi zilizoendelea zimefanikiwa kufikia usawa wa kijinsia kwa kuhakikisha wanawake wanashiriki maendenleo pasipokubaguliwa, wanasoma vizuri, hawalazimishwi kuolewa na kutumika kwa starehe kwa ajili ya mwanaume, lakini wanaongoza kwenye taasisi na mashirika mbalimbali. Tanzania tumebahatika kuwa na rais wa kwanza mwanamke kutokana na matakwa ya Katiba, tunaamini kwa uongozi wake jamii inakwenda kubadili mtazamo kuwa inawezekana kuwa na rais mwanamke au kiongozi wa nafasi yoyote wa jinsia hiyo.

Haitakuwa ajabu ikiwa mwaka 2025 atagombea nafasi hiyo kwa mujibu wa Katiba, pia wengi watajitokeza kwenye majimbo na kata pasipo kusubiri viti maalum ambavyo mara nyingi vimeonekana ni namna ya kuwapa wanawake upendeleo na siyo kwa sababu wana sifa za kushika nafasi hizo.

Wengi wanatafsiri tofauti ya wabunge wa viti maalum kuwa ni kama mserereko, ingawa kiuhalisia wanapita kwenye chujio mbalimbali kutokana na sifa na vigezo vilivyowekwa na kila chama, lakini kutokana na matazamo wa jamii wanaonekana hawawezi kusimama kwenye majimbo.

Kujiamini hujengwa kuanzia hatua za malezi kwenye familia na jamii inayomzunguka, baadaye shuleni na kazini, tunaamini ni muhimu kuamini ili kufikia agenda ya Umoja wa Mataifa ya 2030 ya kubadili dunia yenye usawa wa kujinsia na ushiriki wa wote kimaendeleo.

Licha ya mafanikio mengi bado kuna kazi kubwa ya kuhakikisha wanawake wanaongoza kwa mujibu wa sifa na vigezo, kuwa na sera na sheria zinazowezesha usawa wa kijinsia.

Pia ni muhimu kufanya marekebisho ya Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 na Sheria ya Mtoto ili zisipingane na Katiba ambayo ndiyo sheria mama kwenye umri wa mtoto, kwa kuwa katika baadhi ya jamii zimetumika kumwozesha mtoto badala ya kupata haki ya kusoma.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Mbinu hii kukomesha ukatili wa kijinsia ilivyo ya kipekee

**LENGO** namba nne la Kimataifa la Maendeleo Endelevu (SDGs), linagusia usawa wa kielimu, likitaka kuwapo kwa fursa sawa kwa makundi yote kuipata haki hiyo.

Kadhalika lengo la tano linahimiza usawa wa kijinsia. Kwa ujumla yanatetea ustawi na hatima njema ya mwanamke.

Wadau mbalimbali kwa kushirikiana na serikali wanajitahidi kutekeleza malengo hayo.

Kituo cha Taarifa na Maarifa Kipunguni, jijini Dar es Salaam au Sauti ya Jamii, ni miongoni mwa wadau hao, ambao ili kufikia usawa katika elimu kwa kukomesha vitendo vya ukatili wa kijinsia, wanatoa mafunzo na huduma.

Ukeketaji, mimba za ututoni na ndoa za utotoni ni miongoni mwa vitendo ambavyo vinapigwa vita kwa kukamata wanaovisababisha, lakini elimu inatolewa kwa jamii ili kuachana na vitendo hivyo.

Kituo hicho kinatoa elimu ya kupinga vitendo hivyo, katika familia, jamii na hata shuleni maeneo ya Kipunguni, kuokoa mabinti ambapo baadhi yao wamepewa mafunzo ya ufundi bure kwa lengo la kuwawezesha kujitegemea.

Taarifa ya kituo hicho inayotolewa kuhusu mafanikio ya kukabiliana na unyanyasaji huo, wakati Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum Dk. Dorothy Gwajima, anapotembelea Sauti ya Jamii, inamvutia.

Anaagiza kufanyiwa makala maalumu kwa ajili ya kusambazwa ili kuigwa na wadau wengine wanaofanya kampeni kama hizo.

Ni katika ziara yake hivi karibuni kwenye kata ya Kipunguni akihamasisha watu kujitokeza kwa wingi katika maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani na kupewa taarifa za maendeleo ya kituo hicho.

Taarifa hiyo iliyosomwa na mwenyekiti wa kituo, Fatma Talib, inaonyesha jinsi ambavyo mafunzo ya ufundi kwa watoto wa kike waliokimbia ukatili na kutoa elimu ya kupinga ukatili wa kijinsia shuleni na majumbani yalivyoleta tija, jambo linalomkuna zaidi Waziri Gwajima.

Mwenyekiti huyo anasema, tangu kianze kutoa mafunzo ya ufundi cherehani bure mwaka 2016, kimesaidia wasichana 360 waliokimbia ukeketaji kutoka nyumbani kwao ambao sasa wanajitegemea.

Mbali na ufundi chereheni mafunzo mengine ni ya saluni na ujasiriamali kwa wanawake walioacha ungariba ambao pia wamepewa mbegu na vitalu ili kulima mboga za majani na kuziuza katika masoko mbalimbali.

Fatma anasema, kituo hicho kiko chini ya Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), huku kikisaidiwa na baadhi ya wadau kama Women's Legal Aid Centre (WILAC), Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu Duniani (UNIFPA), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), Women Fund Tanzania (WFT) na Timiza, Binti Makini.

Hatua ya kumnyima elimu mtoto wa kike au wa kiume, ni miongoni mwa vitendo ambavyo huchukuliwa kama ukatili wa kijinsia, ambao kituo hicho kinapambana nao kwa kuelimisha jamii ili ibadilike.

Kimsingi, juhudi zinazofanywa na kituo hicho, ni vyema zikaungwa mkono na wadau wote wanaopenda maendeleo ya mtoto wa kike ili kukomesha vitendo vyote vinavyomkwamisha.

Juhudi hizo zikipewa kipaumbele na jamii, ninaamini kuwa kaulimbiu ya maadhimisho hayo kwa mwaka huu isemayo; 'Kizazi cha Usawa wa Kijinsia kwa Maendeleo Endelevu inaweza kuzaa matunda.

Kaulimbiu hiyo pia inamalizia kwa kuhamasisha jamii kujitokeza kuhesabiwa katika sensa ya watu na makazi inayotarajiwa kufanyika mwaka huu. Lakini binafsi ninataka kukazia zaidi suala la usawa wa kijinsia kwenye elimu.

Usawa katika elimu ni muhimu, lakini usawa huo huanzia nyumbani, kwa lengo la ufikiaji wa elimu kwa wasichana na wanawake, hivyo ni vyema jamii ikashiriki kikamilifu kuhakikisha jinsi zote zinapata elimu kwa usawa.

Wazazi na walezi ni muhimu watambue majukumu wanayowapa watoto wao na maadili wanayowasilisha kwao kwa kuelimisha kuhusu usawa wa kijinsia ikiwamo kuwafahamisha kuwa wote wana haki sawa katika kupata elimu.

Ni vyema wanawake wanapoadhimisha siku hii, waangalie uwezekano wa kuongeza vituo vingi zaidi kama hicho cha Kipunguni, ili elimu ya kukomesha vitendo hivyo usamba kote nchini hasa maeneo ya pembezoni.

## 15 mbaroni kwa tuhuma za mauaji

Na PENDO THOMAS, KIGOMA

JESHI la Polisi mkoa wa Kigoma linawashikilia watu 15, akiwamo Mwenyekiti wa Kijiji cha Kagerankanda, Tamsano Nyandula, kwa tuhuma za mauaji ya watu wawili.

Watu hao waliuawa wakituhumiwa kujihusisha katika matukio ya kuwabaka wanawake watatu kwa nyakati tofauti walipokuwa wakiokota kuni porini na kutafuta uyoga.

Kamanda wa Polisi mkoa wa Kigoma, ACP James Manyama, alisema mauaji hayo yalifanyika Februari 28, mwaka huu na kwamba aliyeuawa ni Devile Emmanuel (31), raia wa Burundi na mwenzake ambaye jina na makazi yake havijatambuliwa.

Manyama alieleza baada ya uwapo wa matukio ya ubakaji, mwenyekiti wa kijiji hicho aliungana na wananchi katika msako wa kuwatafuta wahusika ndipo waliwakamata watu hao wawili waliokuwa wakifanya shughuli za kilimo katika Msitu wa Makere kisha kuwashambulia kwa kutumia silaha za jadi katika sehemu mbalimbali za miili yao.

Aidha, alieleza kuwa Machi 6 lilitokea tukio lingine la mauaji ya kijana Baraka Syekeye (22), mkazi wa kijiji cha Mwayaya Wilaya ya Buhigwe ambaye aliuawa kwa kushambuliwa na marungu, fimbo na mawe baada kukutwa akiiba betrii za solar katika Zahanati ya Mwayaya.

"Niwaombe viongozi wa serikali za vijiji na mitaa, wasiwe vyanzo vya kuhamasisha wananchi kukiuka sheria na kusababisha matukio ya mauaji," alisema Manyama.

Kamanda huyo alisema uchunguzi unaendelea na ukikamilika watu hao 15 watafikishwa mahakamani, huku akiahi kuwa jeshi hilo litawasaka wahusika waliofanya mauaji ya kijana Baraka katika kijiji cha Mwayaya wilayani Buhingwe.

# Balozi wa Msumbiji ahimiza vijana kuendeleza talanta zao

Na Mwandishi Wetu

BALOZI wa Msumbiji hapa nchini, Ricardo Amrosio Mtumbuida, amewataka vijana wa kitanzania kujenga tabia ya kuziendeleza talanta zao kama njia mojawapo ya kujipatia kipato cha uhakika na kuondokana na dhana ya kusubiri kuajiriwa.

"Wakati umefika kwa vijana kuanza kuzitambua talanta ambazo Mungu amewapa na kuzibadilisha kuwa fursa ambazo zitawasaidia kubadilisha maisha yao sambamba na kuondoka na dhana ya kusubiri kuajiriwa," Alisema Balozi Mtumbuida.

Akizungumza mkoani Dar es Salaam kwenye uzinduzi wa vitabu viwili vya Kiingereza vya 'A day with a Quote na Dear Paula' ambavyo viandikwa na Mshairi chipukizi, Aisha Kingu, alisema ni wakati wa vijana kutumia talanta zao kujiajiri ili wajikwamue kiuchumi kwani zipo fursa lukuki zimefichwa kwenye talanta za vijana.

Alitoa pia wito kwa wazazi kuwa mstari wa mbele kuhakikisha kuwa wanazitambua talanta za watoto wao na kuziendeleza ili ziwe mkombozi kwa siku za usoni kwa kujitengenezea kipato cha uhakika.

''Wazazi wapo katika nafasi nzuri sana ya kuziendeleza talanta za watoto wao tangu wanapozaliwa. Napenda pia kumpongeza Dkt. Saidi Kingu kwa kutambua talanta ya binti yake na kumsaidia kufikia malengo na kutimiza ndoto zake," alisema.

Kwa upande wake, mwandishi wa vitabu hivyo, Aisha, alisema vitabu hivyo vimebeba ujumbe mbalimbali na kila atakayesoma vitabu hivyo vitampa msukumo na nguvu ya kukabiliana na changamoto pamoja na mtazamo chanya katika kufikia mafanikio.

"Ukiangalia kitabu cha Dear Paula, ni kitabu kilicholenga kumpatia uhuru wa kipato binti kupitia ujasiriamali ambapo tunaona barua ya mama kwenda kwa mtoto inayompa muongozo na njia katika safari ya ujasiriamali sambamba na kumkumbusha yeye ni nani na anapaswa kufanya nini ili kufikia mafanikio," alisema Aisha na kuongeza kuwa A Day with a Quote ni kitabu ambacho kimebeba dhima ya msukumo, kutia moyo na motisha.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ushindani wa Haki (FCC), William Erio, aliwapongeza wazazi wa binti huyo na kuwaasa wazazi wengine kuiga mfano huo na kuwa chachu katika kuendeleza vipaji vya watoto wao kwani kwa kufanya hivyo watoto watapa uhuru na ufanisi zadi kiutendaji badala ya kuwalazimisha kufanya wasiyoyataka.

''Nipende kuwaasa wazazi wezangu kuiga mfano wa wazazi wa Aisha Kingu kwani walitambua talanta ya binti yao na kuiendeleza na sasa amekuwa akipeperusha bendera ya Tanzania ndani na nje ya Tanzania kwa talanta tu." alisema Erio.

Bi. Aisha mbali ya kuwa mwandishi wa vitabu na mtunzi wa mashairi ni mwanasheria na wakili pamoja umri wake mdogo amejizolea umaarufu mkubwa kwa kuwaandikia mashairi viongozi wa ndani ya nchi na nje ya Tanzania akiwemo Rais mstaafu wa awamu ya nne Dk. Jakaya Kikwete, Rais wa Urusi Vladimir Putin na Malikia Elizabeth wa Uingereza.




Balozi wa Msumbiji nchini, Ricardo Amrosio Mtumbuida (katikati), akizindua vitabu vya A day with a Quote na Dear Paula vilivyoandikwa na mshairi chipukizi, Aisha Kingu (watatu kushoto), kwenye hafla ya uzinduzi iliyofanyika Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Wapili kushoto ni Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ushindani wa Haki (FCC), William Erio. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kiwanda cha kuunda malori sasa kujengwa nchini

Na Romana Malya

KATIKA jitihada za kuendeleza sekta ya usafirishaji, kampuni ya uuzaji na utengenezaji wa magari ya kusafirisha mizigo ya Sinotruk International, mwaka huu inatarajia kujenga kiwanda cha kuunda magari ya kusafirisha mizigo ili kurahisisha shughuli za wafanyabiashara.

Hayo yalisemwa jana wakati kampuni ya GSM kupitia kampuni yake ya usafirishaji ya Galco Limited ikikabidhiwa malori mapya zaidi ya 100 kutoka kwa kampuni ya uundaji malori ya Sinotruk International.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa hafla fupi ya makabadhiano ya magari hayo, Meneja Mkuu wa kampuni ya Sinotruk International Tanzania, Li Zhongyuan, alisema kuwa mwaka huu Kampuni ya Sinotruk and Saturn Corporation inatarajia kujenga kiwanda cha uundaji wa vifaa vya malori.

"Kiwanda hiki kikianza shughuli zake, kinatarajia kuzalisha ajira takribani 500 kwa Watanzania na kukuza maendeleo ya sekta ya magari Tanzania. Siku zote Sinotruk inaendesha shughuli zake kwa kuzingatia kuwapatia wateja wake huduma bora na za kisasa, bidhaa na huduma zenye ubora wa hali ya juu na kwa pamoja kutengeneza mazingira bora kwa vizazi vijavyo vya Tanzania."

Ofisa Biashara Mkuu wa GSM, Allan Chonjo alisema wameongeza malori mengine mapya na kufikia 800 na kupitia Galco wamekuwa wakifanya usafirishaji wa mizigo ndani na nje ya nchi kwa takribani miaka 10 sasa.

"Nchi zinazohudumiwa ni; DRC Congo, Msumbiji, Malawi Zambia, Burundi, Rwanda, Uganda, Kenya Pamoja na Sudan ya Kusini. Galco ina ofisi tatu, Tanzania, Zambia Pamoja na Afrika kusini hivyo nchi zote za Afrika Mashariki na Kati Pamoja na za ukanda wa SADC zinahudumiwa kwa ufanisi mkubwa," alisema Chonjo.

Aliishukuru serikali kwa kufungua fursa na kuendelea kuimarisha uhusiano ya nchi na majirani.

"Isingekuwa rahisi kwetu kuweza kuingia na kutoka kwenye nchi za watu bila bugudha kama uhusiano wetu na nchi hizo usingekuwa mzuri. Matokeo yake na sisi tunatoa fursa kwa wadau wengine ikiwamo ajira, ubora wa huduma na kuongeza pato la taifa," alisema.

# SIKU YA WANAWAKE DUNIANI





Agness Lema (Collection Executive-Circulation)

Aisha Hassan Madeni (Circulation Officer)

Alice Nyungi (Booking Officer-Finance)

Angel Navuri (Supplement Manager-Advertising)

Winnie Nkya (Regional Sales Executive Iringa)

Augusta Njoji (Reporter- Nipashe Dodoma)



Beatrice Bandawe (Managing Editor Nipashe)

Bahati Hoza (Sub Editor - The Guardian)

Blandina Buluda (Personal Secretary)

Chiku Mbonde (Billing Clerk - Finance)

Diana Mbowe (Operation Executive -Finance)

Dorcus Sembuli (Booking Executive)

Doreen Msofe (Assistant Stores Officer)



Sekela Noel Kilembe (Regional Sales Executive Dodoma)

Eliupendo Lema (Customer Relation Officer)

Esther Mwakalobo (Regional Sales Executive - Mbeya)

Evodia Mbilinyi (Sales Supervisor -Circulation)

Fatma Nizamdin (Data Entry- Finance)

Felister Peter (Chief Reporter-The Guardian)

Getrude Mbago (Reporter-The Guardian)



Josephine Komba (Telephone Operator)

Jophanes Cornelio Muro (Administrative Assistant)

Nuruzeni Masoudi Msangi (Circulation Field Officer)

Heavens Mrema (Regional Sales Executive - Arusha)

Rehema Shedrack Songoro (Administrator)

Grace Moses Laizer (Regional Sales Executive Mwanza)

Martha Mwasyeba (Circulation Field Officer)



Khadija Ngululu (Library Assistant)

Latifa Abdallah (Proof Reader)

Latifa Mnunduma (Office Attendant)

Grace Mfuru (Returns Officer)

Mary Masaki (Returns Officer)

Mary Mbikilwa (Accounts Assistant)

Mary Mwenga (Security Guard)



Somoe Ng'itu (Senior Reporter)

Naila Mhuyuka (Cashier - Finance)

Jenifer Julius Gilla (Reporter)

Rahma Ally Salum (Cashier - Finance)

Rahma Suleiman (Reporter Zanzibar)

Grace Nacksso (Graphics Designer)

Romana Mallya (Reporter)



Violet Msaki (Editorial Secretary)

Sophia Lema (Sales Executive and Special Vendor-Circulation)

Merina Chahali (Booking Officer-Finance)

Angelina Hungu (Security Guard)

Dotto Lameck (Digital)

Salome Kitomary (Senior Reporter)

Sabila Suleiman (Office Attendant)

## CCM: Safari za Samia nje fursa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga, kimewataka wanachama wake kujua kuwa safari za nje zinazofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan ni kutafuta fursa zitakazowafanya wananchi kupata maendeleo ya haraka.

Chama hicho kimesema kwa sasa Watanzania wote wanatakiwa kumuunga mkono Rais Samia kwani amekuwa mstari wa mbele katika kutafuta fursa za kimaendeleo nje ya nchi wakiwamo wawekezaji ambao watasaidia Watanzania wengi kuwa na kipato watakapoanza kuwekeza.

Hayo yalisemwa na Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Kahama, Thomas Muyonga, wakati wa uzinduzi wa kadi za kisasa (kielektroniki) za chama hicho katika Kata ya Segese Halmashauri ya Msalala, huku akiwataka wanachama kuwa na imani na kile anachokuwa akikifanya Rais katika kipindi hiki.

Alisema katika kumuunga mkono Rais Samia, wanachama wa CCM hawapaswi kuyumbishwa na watu wanaobeza kazi zinazofanywa kupitia vijiwe vya kahawa.

"Rais wetu tumuunge mkono katika jitihada zake za kuleta maendeleo kwani katika kipindi chake tayari amefanya mengi ikiwamo ujenzi wa madarasa katika maeneo mbalimbali ili kuhakikisha kuwa kila mtoto wa kitanzania anapata elimu kwa wakati," alisema Myonga.

Aidha, alisema kuwa nchi nyingi duniani ambazo zimekuwa zikiongozwa na wanawakae zimekuwa zikifanya vizuri hasa katika masuala ya utawala bora na kufanya jamii husika kuwa na ustawi mkubwa wa maendeleo.

Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM Wilaya ya Kahama, Joakimu Simbila, alisema, chama kimeamua kuzindua kadi za kisasa ambazo zitakuwa zikiwasaidia wanachama wake katika mambo mbalimbali, ikiwamo kutunza fedha zao.

# RC Mjema ataka jukwaa uwezeshaji wanawake

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, amesema ufanyike mchakato wa kuanzisha jukwaa la kuwezesha wanawake kiuchumi ili waweze kutumia fursa za madini, kilimo na ardhi ambavyo vimekuwapo, lakini hawavitumii.

Mjema aliyasema hayo alipokuwa mgeni rasmi wakati wa kufungua kongamano la wanawake wa mkoa wa Shinyanga ambapo alisema wapo wanawake ambao wamekuwa wakipata shida kujinyanyua kiuchumi na kupata haki zao.

Mjema alisema familia imekuwa ikimtegemea mwanamke, hivyo kuna kila sababu ya kujumuika pamoja na kuanzisha jukwaa la kuwezesha wananchi kiuchumi kwani fursa kwa mkoa huo zipo nyingi.

"Ninataka kuona mwanamke anayetangazwa kufanya biashara vizuri ndani na nje ya nchi awe mwanamke kutoka mkoani Shinyanga, hivyo msisitize pia watoto wasome nakufikia malengo wanawake tunaweza na kongamano hili linawafanya wanawake kuwaunganisha, kufurahi na kubadilishana mawazo," alisema Mjema.

Mjema aliwataka wanawake wachangamkie fursa za miradi mikubwa inayotekelezwa mkoani hapa kama vile uwepo wa nishati ya umeme, reli ya kisasa (SGR) na bomba la mafuta pamoja na uwanja wa ndege ambao upo kwenye harakati ya kufufuliwa ifikapo Juni mwaka huu.

Mjema alisema kuwa kila wilaya atahakikisha wakuu wake wanaanzisha majukwaa ya uwezeshaji wananchi kiuchumi na kuyasimamia ipasavyo ili wanawake watambue fursa na kujifunza kwani watakuwapo wawezeshaji waliobobea kwenye majukwaa hayo.

Ofisa Biashara Manispaa ya Shinyanga, Milembe George, alisema kuwa kuwapo kwa fursa hizo zitawafanya wanawake kupata ajira, kutangaza biashara zao na kukuza masoko ya bidhaa na mitaji ili kujinyanyua kiuchumi.

Baadhi ya wanawake waliohudhuria kongamano hilo, Scholastical Pambaya na Zawadi Kisesa walisema kuwa fursa zilizosemwa na mkuu wa mkoa zipo nyingi, ila wanawake wamekosa elimu zaidi ya kuzitambua, hivyo majukwaa yakija itakuwa fursa kwa wanawake kujikwamua.



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, akizungumza jana kwenye kongamano la wanawake mkoani humo, na kuwataka wachangamkie fursa zilizoko mkoani Shinyanga na kujikwamua kiuchumi, ikiwamo uchimbaji madini, kilimo, ufugaji wa mifugo, pamoja ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) ambayo inapita mkoani humo. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Halmashauri yakopesha makundi maalum mil. 269/-

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

HALMASHAURI ya Ushetu wilayani Kahama mkoani Shinyanga, imetoa mikopo ya Sh. milioni 269 katika vikundi 30 vya ujasiriamali vijana, kinamama na watu wenye ulemavu, kwa ajili ya kuinua mitaji yao, kukuza uchumi na kuondokana na utegemezi kwenye familia.

Ofisa Maendeleo wa Jamii wa Halmashauri hiyo, Morgani Mwita, aliyabainisha hayo wakati wa utoaji wa mikopo hiyo ambapo alisema kila mwaka wa fedha halmashauri imekuwa ikitenga fedha kupitia mapato yake ya ndani kwa ajili ya kuvinua vikundi vya ujasiriamali viliyoko kila kata.

Alisema, wametoa mikopo ya Sh. milioni 269.07 katika vikundi 30 vya ujasiriamali kati ya hivyo vikundi 22 vya kinamama vimepokea Sh. milioni 143.270, vikundi nane vya vijana Sh. milioni 71.3 na watu wawili binafsi wenye ulemavu wamepokea Sh. milioni 4.5 fedha ambazo zimetolewa kwa kipindi cha Julai mwaka 2021 hadi Machi 2, mwaka huu.

Hata hivyo, Mwita alisema, vikundi vya vijana vimekuwa vikisumbua wakati wa urejeshaji wa mikopo hiyo, ili kuvipatia fursa vikundi vingine kukopa ukilinganisha na vikundi vya kinamama na watu wenye ulemavu, na kwamba tabia hiyo inasababisha wachukuliwe hatua kuvichukulia hatua za kisheria.

Naye Mwenyekiti wa Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi Ushetu, Juliana Shayo, alisema, watakutana kwa pamoja ili kujadili vikwazo wanavyokumbana navyo ikiwamo na njia za kuvitatua ikiwamo kuelimishana juu ya matumizi sahihi ya fedha za mikopo ambazo wamekuwa wakipokea kila mwaka.

Katibu wa kikundi cha Umoja ni Nguvu Kata ya Bukomela, Betha Bugaywa, alisema, kila wanapokutana wamekuwa wakikumbushana juu ya matumizi sahihi ya fedha wanazozipata na kwa mwanakikundi anayekwenda kinyume wamekuwa wakimwajibisha kisheria ili asije kuwakwamisha wakati wa marejesho.

Mbunge wa Ushetu, Emmanuel Cherehani, aliwataka wajasiriamali wanawake kuacha tabia ya kuwahonga wanaume wao fedha wanazokuwa wamekopeshwa na halmashauri hiyo kwa ajili ya kujiinua kiuchumi na badala yake wazielekeze katika shughuli walizokuwa wamekusudia kuzifanya.

# Mahakama yaeleza jinsi inavyoendesha mashauri

**Na Said Hamdani,** LINDI

MAHAKAMA imesema utekelezaji kazi za mahakama mara nyingi huzingatia na kufuata sheria, kanuni, taratibu na miongozo iliyowekwa kwa mujibu wa nchi husika katika uwendeshaji mashauri yanayofikishwa na kusaidia kufikia uamuzi wa utoaji wa haki.

Hayo yalielezwa na Hakimu Mkazi Mfawidhi Mwandamizi wa Mahakama ya Mkoa wa Lindi, Consolata Singano, alipokuwa anafungua mafunzo kuwajengea uwezo baadhi ya watendaji wa serikali inayojumuisha Idara ya Ulinzi na Usalama, yaliyofanyika mjini Lindi.

Idara hizo ni pamoja na waendesha mashtaka Taifa ngazi ya mkoa, Jeshi la Polisi Kitengo cha Upelelezi, Magereza, Uhamiaji, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na Mamlaka ya Udhibiti wa Wanyamapori {TAWA} kutoka wilaya zote tano za Mkoa wa Lindi.

Singano alisema watendaji wanapopeleka mashauri mahakamani hutarajia mtuhumiwa kuchukuliwa hatua, bila kutambua mahakama ni chombo kinachojihusisha na masuala ya utoaji haki na sio upendeleo.

Alisema mahakama ni chombo kisicho na huba, na hakina upendeleo, kwani hufuata sheria vikiwamo vielelezo na ushahidi uliofikishwa mahakamani ujitosheleze, hivyo wasitarajie kupata matokeo wanayoyategemea.

Aliwataka waendesha mashtaka, maofisa uchunguzi na wanaohusika na ufuatiliaji haki mahakamani kutekeleza shughuli zao kwa uweledi pamoja na kuzingatia taratibu zinazowaongoza bila kufanya makosa ili haki itendeke.

"Ni muhimu ushahidi ukashikwa kuanzia hatua za mwanzoni kabisa na ukafikishwa mahakamani katika kiwango kinachostahili ili matarajio ya mifumo iweze kutekeleza majukumu yake," alisema Singano.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, Foka Diinya, aliwataka washiriki wa mafunzo hayo kuzingatia kila kitakachofundishwa, huku akiwasisitiza kutosita kuhoji maeneo yote ya kisheria wanapoona kuna utata na kuwaletea shida katika utendaji wao.

Dinya aliwakumbusha washiriki hao kwamba huu ni ulimwengu wa sayansi na teknolojia, hivyo wanaweza kupata mambo mapya zaidi kwani mara nyingi sheria zimekuwa zikitungwa na zingine kubadilika mara kwa mara.

Mkuu wa mashtaka Mkoa wa Lind, Abdurahamani Mohamed, alisema lengo la mafunzo ni kujengeana uwezo kwa makundi yanayoshiriki kufanyakazi chini ya jukwaa la haki jinai, kwani wao ndio watekelezaji wa sheria za kijinai zilizotungwa nchini.

Pia alisema mafunzo hayo yatagusa kuanzia kukamata watuhumiwa au washtakiwa na vielelezo vyao, kufungua mashtaka, jinsi ya kutunza eneo la tukio na vielelezo vinavyokamatwa, kushughulikia mashahidi na kufikisha mahakamani.




ASP Fatma Mtalimbo kutoka Dawati la Jinsia katika Jeshi la Polisi akiendesha semina kwa wafanyakazi wanawake wa kampuni ya Barrick katika kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani. Mafunzo haya yaliyoandaliwa na kampuni yamefanyika katika migodi ya Bulyanhulu na North Mara. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## DC afunda wanawake kuchapa kazi kwa bidii

**Na Neema Hussein,** KATAVI

MKUU wa Wilaya ya Mpanda mkoani Katavi, Jamila Yusufu, amewataka wanawake kuendelea kufanya kazi kwa bidii, weledi, maarifa, juhudi, nidhamu na uaminifu kila mmoja kwa nafasi yake ili kufikia malengo waliyojiwekea.

Jamila aliyasema hayo jana wakati akizungumza na kikundi cha Wanawake Tuzungumze Katavi, huku akiwataka kuchangamkia fursa za maendeleo zinazojitokeza mbele yao bila kubagua.

Jamila alisema maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani yanayofikia kilele leo, yanaenda sambamba na mwaka mmoja wa uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, hivyo aliwataka wanawake hao kuendelea kumuunga mkono kutokana na mambo makubwa anayoendelea kuyafanya nchini.

"Wanawake tuna nafasi kubwa sana kuhakikisha amani inaendelea kudumu na katika shamrashamra za kuelekea siku hii, pia tunaadhimisha mwaka mmoja wa Mama Samia Suluhu Hasan, na kama mmegundua wanawake sasa hivi tunaheshimika sana ni kwa sababu ya mama (Samia)," alisema Jamila.

Jamila aliwataka pia wanawake kujitokeza kuhesabiwa wakati wa sensa ya watu na makazi kutokana na taarifa hizo kuisaidia serikali kufanya maamuzi katika maendeleo ya Taifa, huku akiwasisitiza kuwaelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa sensa.

Jamila aliwapongeza Mwenyekiti na Katibu wa kikundi cha Wanawake Tuzungumze Katavi Yustina Tizeba na Restuta Nyondo pamoja na waandaaji wengine kwa kuwakusanya wanawake sehemu moja na kuzungumza mambo yanayowahusu kwa masilahi yao na Taifa kwa ujumla.

Naye Judith Mbukwa kutoka Kitengo cha Dawati la Jinsia na Watoto Mkoa wa Katavi, alisema wanawake wasiwaadhibu watoto kupita kiasi huku akiwataka kutenda haki kwa watoto wote hasa wale wanaoishi na watoto wa waume zao waliozaliwa na wanawake wengine.

# Wajasiriamali wanawake washauriwa kuhusu vifungashio na vipimo sahihi

**Na Joseph Mwendapole**

WAJASIRIAMALI wanawake wameshauriwa kuendelea kuboresha vifungashio na kuzingatia vipimo sahihi ili bidhaa zao ziweze kukubalika hata kwenye masoko ya kimataifa.

Wito huo ulitolewa jana na Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Vipimo (WMA), Stela Kahwa, wakati akizungumza kwenye maonyesho ya pili ya wafanyabiashara wanawake yaliyoandaliwa na Chama cha Wafanyabiashara Wanawake (TWCC).

Alisema ili bidhaa zao ziweze kuvuka mipaka na kushindana kimataifa hakuna namna ambavyo wanaweza kukwepa kuboresha vifungashio na kuzingatia vipimo sahihi kwenye bidhaa zao.

"Kwenye haya maonyesho ya pili nimeona tofauti kubwa sana kulinganisha na maonyesho yaliyopita kwasababu wengi wametumia mafunzo tunayowapa kuboresha ufungashaji na wamejitahidi kuzingatia usahihi wa vipimo ila waendelee kuboresha zaidi," alisema Kahwa.

"Tumeona makosa madogo madogo kwenye bidhaa zao ambayo yanavumilika na kufundishika na naamini kwa mafunzo tutakayoendelea kuwapa kwenye maonyesho yajayo wataboresha zaidi," alisema.

Alisema WMA mbali na kuwapa mafunzo wajasiriamali hao imekuwa ikiwafuatilia kwenye maeneo yao kujua wanavyoendelea na kuwajengea uwezo pale wanapoona wamekwama.

Alisema WMA kupitia Ofisi zake zilizoko maeneo mbalimbali nchini imekuwa ikiendelea kuwahamasisha wajasiriamali hao wanawake kwa wanaume kuendelea kujitokeza ili kupewa elimu hiyo ambayo manufaa yake ni makubwa.

Alisema kwa kutumia matakwa ya vipimo inayotumika katika soko la dunia nzima, WMA imekuwa ikiendelea kuwapa wajasiriamali hao elimu hiyo kwa lengo la kukidhi matakwa hayo na hivyo kutoa ushindani unaohitajika.

Aidha, alisema WMA itahakikisha inaendelea kutoa mchango wake mbalimbali kwa wajasiriamali hao huku ikiwataka kutumia maonyesho hayo ya kuelekea Siku ya Wanawake Duniani kwenda kupata elimu ya vipimo na ufungashaji.

Mmoja wa wajasiriamali wanaoshiriki maonyesho hayo, Angela Sylivester, alisema maonyesho hayo yamekuwa muhimu kwao kwani wamekuwa wakikutana na wenzao na kubadilishana ujuzi.

Aliomba serikali na wadau mbalimbali kuendelea kuthamini kazi zinazofanywa na wajasiriamali wazalendo badala ya kuthamini zile zinazotoka nje kwani kwa kufanya hivyo watawainua kiuchumi.

Aliomba pia wajasiriamali hao wawe wanapewa mafunzo ya mara kwa mara kuhusu namna bora ya kufungasha bidhaa hizo na kuzingatia vipimo sahihi ili bidhaa zao ziweze kukubalika kimataifa.

Nipashe
# TESA
Jumanne Machi 8, 2022
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 12

## Kinamama wa Zanzibar bega kwa bega uchumi buluu, bidhaa jongoo



Ukurasa 13



Mama msomi aliyepenyeza mabinti lukuki UDSM

## KILELE SIKU YA WANAWAKE



Ni 'Super Woman' wa Tanzania, Rais Samia Suluhu Hassan. Mama wa misingi ya haki, mtumishi wa wanyonge, mtetezi wa kila mmoja kwa usawa wa kijinsia...kazi inaendelea kwa kasi.



**Asha- Rose Migiro**, hawezi kusahaulika kwenye orodha ya viongozi wa dunia, alikuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN) wa kwanza mwanamke na kutoka Afrika.



**Getrude Mongella**, anatisha kiuongozi, ameshika nyadhifa nyingi ni Rais wa kwanza wa Bunge la Umoja wa Afrika. Kuanzia 1993 hadi 1995, alikuwa Katibu Mkuu wa Mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Masuala ya Wanawake uliofanyika Beijing China mwaka 1995 kwa mafanikio.



Katibu Mkuu Kiongozi SMZ, **Zena Ahmed Said**, yuko makini na mahiri kuonyesha kuwa wanawake wanaweza.



Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, **Dk. Stergomena Tax**, ameandika historia SADC akiwa ni mwanamke wa kwanza kuwa Katibu Mkuu wa Jumuiya ya SADC.



**Nenelwa Mwihambi** ni Katibu wa Bunge wa kwanza mwanamama, amedhihirisha umahiri uongozi wa muhimili muhimu wa dola.



**Profesa Esther Mwaikambo** ni daktari wa kwanza mwanamama nchini, tena ni bingwa wa magonjwa ya watoto, anadhihirisha kuwa wanawake hawajawahi kushindwa sayansi.

NA RAHMA SULEIMAN,
ZANZIBAR

# Kinamama wa Zanzibar bega kwa bega uchumi bluu, bidhaa jongoo

• Waamka usiku kwenda baharini • Bei yawakosha, kilo Sh. 100,000 • Dk. Mwinyi awaelekezea mikopo

LEO ni kilele cha Siku ya Wanawake Duniani, ambayo katika mustakabali mpana inaangalia kukomboka kiuchumi. Nadharia hiyo Visiwani Zanzibar, inajikita moja kwa moja uliko uchumi wa bluu, ambao ni sehemu ya mzizi wa maisha yao.

Unapptajwa uchumi wa bluu, ni shughuli inayojumuisha uvuvi, utalii, usafiri baharini, ujenzi wa bandari za kisasa, kilimo cha mwani, ufugaji majongoo pwani, uchimbaji mafuta, gesi na matumizi ya rasilimali za bahari kwa kuzingatia uhifadhi mazingira.

Hapo napo kwenye shughuli hiyo inayotimiza muongo mmoja tangu kuanza Zanzibar, kunaibuka jingine kwenye sura ya mgawanyo kijinsia. Ushiriki wa wanaume unaonekana kuchukua kasi wakionekana kwa wingi katika uzalishaji wake, huku kinamama idadi yao hairidhishi, hata kuugusa uongozi wa juu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ).

Alipofungua kongamano la wanawake kuhusu nafasi yao katika kukuza uchumi wa bluu, lililoandaliwa na Benki ya Taifa ya Biashara (NBC), Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi, amewataka wanawake kuchangamkia fursa za uchumi wa bluu, badala ya kuwaachia wanaume pekee.

Katika hilo, Rais Dk. Mwinyi anasema wanahitajiwa kupewa elimu ya namna ya kuitumia fursa hiyo kwa sababu baadhi yao wanadhani uchumi wa bluu, ni mahsusi kwa wanaume pekee.

Pia anasema tayari ameshaielekeza Wizara ya Fedha na Mipango ya SMZ kufanya mazungumzo na Benki ya TCB, ili kuwawezesha wajasiriamali hasa wanawake wasisumbuliwe na serikali athamini juhudi za wanawake katika kuendeleza mazao ya baharini ambayo ni sehemu ya uchumi wa bluu.

Wakati Zanzibar hadi sasa inatajwa kuwa nchi ya pili ukanda wa Afrika katika kuanzisha ufugaji viumbe bahari wakiwamo majongoo, Nipashe iliamua kuwahoji kinamama wanaoshiriki uchumi wa bluu na kupata maini yao:

### KINAMAMA NA MAJONGOO

Semeni Muhammed, ni mama wa watoto wanne na amejikita katika ufugaji majongoo, akikiri uwiano wa kijinsia katika uchumi wa bluu bado ni mdogo kinamama wachache na sababu kuu ni wao kukosa mitaji.

Anasema asilimia 85 ya wanawake Zanzibar wamejikita katika kilimo cha mwani, wanaume wanakimbia kilimo hicho kutokana na changamoto zake ikiwamo gharama kubwa za uzalishaji na kipato chake kidogo, ikilinganishwa na uchumi wa bluu.

Semeni anayeishi Mjini Unguja, anasema anmeanza kufuga majongoo mwaka 2016, akipitia changamoto nyingi ikiwamo ya mtaji, akiamini akipata mtaji atafikia mapinduzi ya mapato.

"Ili uwe na shamba la kufuga majongoo ya bahari unahitaji milioni tano kwa ajili ya maandalizi ya ufugaji, ukianza na kununua vifaranga na vifaa vya ufugaji huo. Inawawia vigumu wanawake wengi kutokana na kipato kidogo japo ni biashara yenye faida kubwa mno," anafafanua.

Semeni kwa sasa ana shamba baharini eneo la Kisakasaka, mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja, anaeleza kilichomvutia katika biashara hiyo ni pale alipogundua thamani kubwa ya majongoo.

"Mwaka 2011 nilifika China na kujionea ufugaji wa majongoo, nilivutiwa sana na ufugaji huu ambao baada ya kurudi Zanzibar, tulianzisha ushirika wa wakulima wa majongoo na mimi katibu wa ushirika wenye wanawake na wanaume," anasema.

Anaendelea: "Tuko wanachama 30, lakini wanawake ni 10 na changamoto kuu katika ufugaji huo ni upatikanaji vifaranga vya majongoo na ulinzi kwa sababu bila ya ulinzi majongoo huibiwa baharini.

"Hii changamoto ya ulinzi ni kubwa sana hasa kwa sisi wafugaji wanawake, kwa sababu muda wote mchana na usiku majongoo yakiwa shambani yanahitaji ulinzi, wanawake tunashindwa kulinda nyakati za usiku hasa maji ya bahari yakijaa."

Harusi Said Ali, anayeishi Kijiji cha Uzi, Kusini Unguja, anasema amevutiwa na ufugaji majongoo bahari, kutokana na hamasa aliyoipata kutoka kwa mumewe na sasa anakiri maisha yamebadilika, hasa kusaidia na kuendeleza watoto kielimu, licha ya ugumu kuamka usiku kwenda kuyahudumia majongoo kabla ya maji kujaa.



Katibu wa Ushirika wa Wafugaji Majongoo, Semeni Muhammed, akionyesha jongoo lililo tayari kuvuliwa, katika shamba darasa, pwani ya Bweleo mkoa wa Mjini Magharibi Unguja. **PICHA: MTANDAO**

> Wavuvi wa mazao ya baharini changamkieni fursa za kilimo cha majongoo ya baharini kwani kinalipa ambapo kilo moja ya najongoo ni Sh. 100,000.

Asha Haji, anayeishi Kijiji cha Fungurefu Mkoa wa Kaskazini Unguja, mwenye shamba la majongoo la ekari mbili, analalamikia ugumu unaowakabili unajumuisha elimu ya ufugaji, mitaji, miundombinu, usalama wa mashamba na vifaa vya kuimarisha uzalishaji huo.

### SMZ VS UCHUMI BLUU

Katibu Mkuu Wizara ya Uvuvi na Uchumi wa Buluu, Dk. Aboud Suleiman Jumbe, anasema kutokana na kuongezeka biashara ya majongoo baharini katika nchi za Bara Asia zikiwamo Singapore, China na Japan, mashirika ya kimataifa yanayojishughulisha na uhifadhi wa mazingira ya baharini wamekuja na mbinu mpya za ufugaji wake, ili kuwa bidhaa endelevu.

Anaeleza Zanzibar ufugaji wa majongoo ulianza katika mwaka 2011 huko Fukuchani mkoa wa Kaskazini Unguja, ambako tija yake ikaonekana kwa wananchi.

"Wavuvi wa mazao ya baharini changamkieni fursa za kilimo cha majongoo ya baharini kwani kinalipa ambapo kilo moja ya najongoo ni Sh. 100,000," anasema.

Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda wa SMZ, Said Omar Shaaban, anasema wameshakamilisha kutunga sheria na sera muhimu kwa maendeleo ya uchumi huo, pia kuna mpango endelevu wenye thamani ya Sh. bilioni 149 kwa ajili ya kuwawezesha wadau wa uchumi wa bluu, wakiwamo wavuvi na wafugaji wa mazao ya baharini.

Shaban anasema, ni sehemu ya fedha za mkopo kwa ajili ya kuimarisha uchumi baada ya kuathirika kutokana na maradhi ya UVIKO-19, huku akifafanua ni mpango unaolenga kuimarisha uzalishaji zao la mwani shambani, samaki na kaa baharini, ikiwa inalenga mikakati ya Dira ya Maendeleo ya SMZ kufikia mwaka 2050; kuwainuwa wakulima wa mazao ya baharini katika uchumi wa buluu.

"Kupitia fedha za ahuweni ya mlipuko wa ugonjwa wa COVID -19 kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) imekamilisha taratibu za ujenzi wa mabwawa 100 ya ufugaji wa majongoo, ili kupatiwa wananchi wa wilaya zote za Unguja na Pemba ambayo yatawekwa miundombinu ya kisasa pamoja na vifaranga vya majongoo hayo," anasema.

NA GAUDENSIA MNGUMI

PROFESA PENINA MLAMA

# Mama msomi aliyepenyeza mabinti lukuki Chuo Kikuu Dar

## • Asubuhi, mchana, jioni anampigania mama

PROFESA Penina Mlama ni 'super woman'. Ni mwanamama wa kwanza kushika wadhifa wa Ofisa Mkuu Taaluma -'Chief Academic Officer -CACO' wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Ni wa kwanza katika wadhifa huo, vyuo vikuu vya Afrika Mashariki na Kati, pengine hata Afrika Kusini ya Jangwa Sahara.

Ni kuanzia 1991 hadi 1998, anakalia kiti cha CACO, haikuzoeleka kukutana na mwanamke kwenye ofisi hiyo lakini ilitokea, ikumbukwe tangu 1964 chuo kilipoanza, wahadhiri wanaume ndiyo pekee walioshika jukumu hilo.

Profesa Peninah ni jina kubwa kwenye maendeleo ya taaluma nchini. Linapotajwa kinachoambatana nalo ni kuinua wanawake kitaaluma kwenye elimu ya juu kwa kuongeza idadi yao vyuoni na kwenye kozi zilizoogopwa hasa sayansi na uhandisi.

Kupigania haki na usawa wa kijinsia kwenye taaluma, ndilo jina la bendera yake. Katika kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani, anazungumza na Nipashe, akisema japo kazi ilikuwa ngumu lakini hata leo, mapambano yanaendelea.



Wahitimu wa vyuo vikuu wanawake wameongezeka zama hizi. Juhudi za kufikia mafanikio hayo zimeanzia na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kupitia mpango kuendeleza usawa wa kijinsia kwenye elimu ya juu. **PICHA: MTANDAO**

### ALICHOACHA UDSM

Anasema katika kipindi cha uongozi wake alihakikisha idadi ya wasichana wanaoingia chuo kikuu inaongezeka. Kwa kuanzisha sera na sheria ya usawa wa kijinsia.

Anasema ili kufanikiwa suala la usawa wa kijinsia, lisiishie kwenye maneno ni lazima kuwe na mikakati ya kubadilisha mifumo na fikra ili iwe ya kiusawa.

"Nilipambana tukaanzisha sera ya usawa wa kijinsia chuoni. Nikawashawishi wenzangu tukaiingiza suala la usawa kijinsia kwenye mpango mkakati wa chuo, ili kufanikisha kuongeza idadi ya wasichana. Tukasema ndani ya miaka mitano tuwe tumefikia asilimia 30. Miaka mingine mitano ijayo tufikie asilimia 50/50 kwenye udahili."

Anaeleza kuwa usawa ulipoingizwa kwenye mpango mkakati wa chuo ulikuwa kama sheria, hivyo yeyote aliyekuja uongozini alilazimika kuufuata.

Anataja data za wasichana waliokuwa wanadahiliwa chuoni ilikuwa chini mno, kwenye vitivo vya sayansi na uhandisi ilikuwa chini ya asilimia tatu, wakati sanaa na sheria alikuwa afadhali kwa asilimia 17.

> "Kwa hiyo tulipoamua kuongeza idadi ya wasichana, kwenye vitivo vya sanaa na sheria haikuwa shida, walikuwapo ila uhandisi na sayansi ilileta shida, hawakuwapo wa kutosha.

Anakumbusha kuwa walivyoweka sheria na mikakati waligundua kuwa walikuwapo wasichana waliokuwa na uwezo na waliofaulu, lakini miaka ya 1990 vyuo vikuu vilikuwa vichache sana na ushindani mkubwa.

Wengi walioomba nafasi lakini hawakudahiliwa, si kwamba hawakuwa na uwezo au sifa, ila nafasi zilikosekana.

"Kwa hiyo tulipoamua kuongeza idadi ya wasichana, kwenye vitivo vya sanaa na sheria haikuwa shida, walikuwapo ila uhandisi na sayansi ilileta shida, hawakuwapo wa kutosha," anakumbusha.

### JICHO KALI SAYANSI

Profesa Penninah anasema kwa sababu kiujumla wavulana na wasichana hawakuwa wengi kwenye tahsusi (combination) za sayansi kitivo hakikupata maombi ya kutosha kujaza nafasi kama kilivyohitaji.

Aidha, idadi ya wasichana waliosoma sayansi ilikuwa chini mno kutokana na changamoto zilizowakwamisha kwenye shule zao za sekondari.

Anatoa mfano kuwa wengi hawakufaulu vizuri, si kwa sababu hawakuwa na akili lakini pengine walikosa walimu.

"Walimu wengi walikuwa ni wanaume, baadhi hawakutaka kufundisha shule za wasichana. Kwa kukosa mwalimu wa fizikia, kemia, biolojia hata kama binti ana uwezo mkubwa hawezi kufaulu vizuri." Anaeleza.

"Kwa hiyo ikabidi kuwe na mkakati wa kuwapata wanaodahiliwa kwenye shahada za sayansi. Nilipigania tukaanzisha programu maalumu ya kuingiza wasichana kwenye sayansi. Tuliita 'pre-entry' program. Tulipata matatizo kiasi, lakini tulisema wasichana watakaoomba kujiunga na sayansi iwapo watakosa pointi za kuingia chuo kikuu, tutawanyanyua," anasema.

Anataja mikakati mingine kama kuangalia alama za mwisho za kuingia UDSM ili kuwainua wasichana, akisema kama pointi za mwisho zilikuwa sita, msichana akiwa na alama 5.5 alichukuliwa.

Waliosajiliwa kwa alama za chini walisomeshwa kwa wiki nane kujifunza sayansi na kufanya mtihani, waliofaulu waliingia chuoni na wengi wamefanikiwa, anasema.

Mpango, uliongeza idadi ya wasichana waliodahiliwa UDSM kusoma sayansi, kadhalika Kitivo cha Uhandisi kikauchukua na kikafanikiwa pia kwani ilikuwa kama sheria, anasema.

### HATUA ZA MAKUSUDI

Profesa Penninah anaziita hatua hizo 'affirmative actions, akisema ni mpango uliotekelezwa na chuo kwa kuamua kuwa wasichana wa kozi zote wataingia chuo kikuu wakiwa na nusu pointi chini ya wavulana, ili kuongeza udahili wao.

"Ushindani ulikuwa mkubwa, vyuo vichache inawezekana mwanafunzi ana daraja la kwanza au la pili lakini anakosa nafasi. Tukaamua wasichana wakipungukiwa pointi kidogo chini ya wavulana tuwape nafasi. Mfano kama kitivo kinasema pointi ya mwisho ya kudahiliwa

INAENDELEA UK.14

## KILELE SIKU YA WANAWAKE

# Mama msomi aliyepenyeza mabinti lukuki Chuo Kikuu Dar

INATOKA UK.13

ni alama saba wasichana wenye pointi 6.5 wachukuliwe, kwa njia hiyo walioingia UDSM waliongezeka." Anaeleza.

Anajisikia fahari leo, vitivo vingi idadi imeongezeka karibu imefikia au kukaribia 50 /50. Sayansi ilikuwa chini asilimia 2.0 sasa wamefika zaidi ya asilimia 25, kwake ni mafanikio makubwa, anasema.

"Naamini tusingeweka sera hiyo tusingelirekebisha udahili na kuongeza wasichana chuoni, ni jambo la kujivuania kwenye maisha yangu. Si hivyo tu hata mamlaka za chuo, serikali na wadau wa elimu ya juu waliona kuwa wasichana au wanawake ni wachache kwenye elimu vyuoni wakaamua kuwapa nafasi na kuwaangalia kwa jicho jingine," anasema.

Kadhalika, anasema kilichofanyika ni kukamilisha mkakati wa kiserikali tangu Uhuru wa kuwapa wanawake nafasi maalumu, licha ya kwamba hakukuwa na utekelezaji, siyo kwamba UDSM iliunda jambo jipya bali ilitekeleza maelekezo.



Profesa Penninah Mlima, mwanazuoni anayejali usawa wa kijinsia ili kuwainua wanawake na wanaume kitaaluma. **PICHA: MTANDAO**

### PENNINAH NA 'PANCHI'

Ofisa Mkuu wa Taaluma, aliongoza UDSM wakati kukiwa na unyanyasaji mkubwa wa wanawake uliokuwa unafanywa na kundi lililojiita 'Mzee Panchi', anazungumziaje?

"Ulikuwa ni unyanyasaji wa hali ya juu wa kijinsia wa wasichana kupitia Mzee Panchi na kusababisha kifo cha msichana mwanafunzi.

"Anasema serikali na uongozi wa UDSM uliipiga marufuku na kuweka sheria na maagizo kuifuta na kuizuia, tena kuweka msimamo kuwa atakayekamatwa na unyanyasaji angefukuzwa chuo.

Mzee Panchi yalikuwa ni mazoea ya kuandika kashfa za ngono, kuchafua na kudhalilisha wasichana wa UDSM kwa kubandika taarifa zao maeneo mbalimbali ya chuo.

"Uongozi wa shule uliridhia, ilikuwa ni unyanyasaji, lakini zilikuwapo rushwa za ngono na unyanyasaji baina ya walimu na wanafunzi, walimu kwa walimu na wafanyakazi wanafunzi wao kwa wao. Mimi na wenzangu tunaotetea haki za wanawake tulipambana sana na hilo," anasema na kuongeza:

"Waliokuwa wanaripotiwa na kuthibitishwa walifukuzwa wakiwamo wahadhiri lakini bado nasikitika pamoja na juhudi zote kupambana na rushwa ya ngono, hata sasa tatizo lipo. Karibuni TAKUKURU wamefanya utafiti

> Nakumbuka siku moja viongozi wa serikali ya wanafunzi wa UDSM - DARUSO, walinifuata ofisini wamechukia sana, wanafoka kupinga 'pre-entry' program, walitaka ifutwe.

na kubaini rushwa ya ngono na unyanyasaji vipo. Licha ya walimu na wanafunzi kufukuzwa bado ni tatizo."

Anasema UDSM ilianzisha na kuweka sera ya kukabili unyanyasaji kingono (sexual harassment policy) na kwamba vyuo vingi vimeiga ili kukabili watuhumiwa wa unyanyasaji.

### JAMBO LILILOMKERA

Anasema kubwa analolikumbuka kwenye harakati zake ni ugumu wa kuwafukuza wahusika wa unyanyasaji kwenye vikao vya nidhamu. Wajumbe ambao ni wahadhiri, wengi walikuwa wanaume na wote walikaa kimya hawakuridhia mwenzao kufukuzwa kazi kwa kosa la unyanyasaji kingono hata ilipothibitika.

Anasema walijua kuwa mwenzao amekosa lakini kwenye vikao lazima kuwe na maamuzi ya wengi na ikifika kwenye kuchukua hatua walikaa kimya ili isipatikane koramu (akidi) ya kusema ndiyo afukuzwe.

" Waliona taabu kufukuzana. Ilikuwa ngumu sana. Watu wazima walikuwa wanakaa kimya wananitazama, ilikuwa inasumbua kudhibiti unyanyasaji na rushwa za ngono," anakumbuka.

### KUKATAA 'PRE-ENTRY'

"Nakumbuka siku moja viongozi wa serikali ya wanafunzi wa UDSM - DARUSO, walinifuata ofisini wamechukia sana, wanafoka kupinga 'pre-entry' program, walitaka ifutwe.

"Nikawaambia ninyi ni DARUSO mna sheria zenu 'by-laws', je kuna inayowapa mamlaka ya kukataza au kufuta mipango au sheria za chuo? Mnapata wapi mamlaka? Nikawauliza wanitajie, nikawataka waniletee sheria hiyo, tena walifika wanaume wenyewe bila kushirikisha wasichana viongozi wa DARUSO."

" Nikambana mmoja nikamuuliza ungekuwa na mdogo wako msichana aliyekuja 'pre-entry,' ungenilazimisha nimfukuze? Nikawaambia angalieni hamtaki wasichana wasome? Kama kuna dada au wadogo zao na jamaa wangetaka wafukuzwe na programu ife?

Anasema aliwakumbusha kuwa ni sheria na taratibu za chuo ambazo zinawezesha Watanzania wote kunufaika haina maana kuiondoa.

Wakasema wasichana wameshindwa na hawawezi kwanini wanawalazimisha kusoma? Nikawaambia: "Nafuatilia maendeleo yao msiseme hawana akali, nikawaambia kwenye sayansi matokeo yao kwenye 'semester' wengi ni 10 bora.

Nikawaambia hiyo programu haitafutwa. Kulikuwa na mapambano kila wakati maana ni jamii yenye mfumo dume.

### NINI KIFANYIKE?

"Wanaopigania haki za wanawake wasiishie kusema ni lazima kuwa na mikakati inayotekelezeka. Kwenye majukuwaa tumeongea kwa miaka 60 tangu Uhuru, tunachotakiwa ni kuvunja mifumo na kutekeleza mikakati tuliyoipanga."

Anasema, anafanya programu ya kuleta usawa wa kijinsia kwenye vyuo vya ualimu na kwamba vingi vina hali inayozuia usawa kijinsia.

"Mambo mengi yaoondoa usawa wa kijinsia kwenye vyuo mfano uongozi, kwenye chuo mkuu, makamu, wakuu wa idara, mshauri wa wanafunzi wote ni wanaume. Safu yote ya uongozi ni wanaume, unashangaa.

"Wanadai hakuna wanawake, lakini kinachokwamisha ni mtazamo ya mfumo.

Ukiangalia kwenye vyuo vya walimu Tanzania viko 35, lakini wakuu wake wanawake ni tisa pekee, kwanini? Ni matokeo ya fika na mitazamo isiyojali usawa."

Anayeteua hafirikirii wanawake, anawaza wanaume zaidi. "Tunachohitaji sasa ni sera na sheria. Kwenye menejimenti lazima iwe 50/50. Kama safu ina watu 10 wanawake watano na wanaume watano."

Anasema tumepiga kelele mitizamo na fikra ya mfumo dume inawaweka wanaume mbele na wanawake nyuma sasa ni kubadilisha mifumo.

Siasa wabunge na madiwani, sheria za uchaguzi zitamke kama jimbo lina kata 10 au 20 utaratibu ni 50/50 hata bunge litunge sheria iwekwe wazi, siyo muda wa kuendelea na asilimia 100 ya wanaume, wanawake nao wapewe nafasi.



## Viongozi waonywa kuuza miche ya miti

**Na Peter Mkwavila,** CHEMBA

WILAYA ya Chemba imekemea tabia ya baadhi ya viongozi wa kata na vijiji kuuza miche ya miti inayotolewa na wadau wa mazingira kwa ajili ya kupanda kwenye maeneo mbalimbali.

Miongoni mwa maeneo hayo ambayo miche hiyo inatakiwa kupandwa ni shule, taasisi za kidini na majengo ya ofisi.

Kaimu Katibu Tawala wa Wilaya hiyo, Rhobi Stephano, alitoa angalizo hilo juzi kwenye maadhimisho ya Siku ya Wanyamapori Duniani yaliyofanyika kimkoa wilayani humo katika kituo cha Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA) kilichoko Pori la Akiba la Swagaswaga.

"Ninasikitishwa sana kuona juhudi zinazofanywa na taasisi mbalimbali zinazotoa miche ya kupanda ikiwamo ya matunda, baadhi ya walimu wanaokabidhiwa wanauza kwa wananchi, badala ya malengo yaliyokusudiwa ninawasihi viongozi wezangu tuache tabia hiyo mara moja na isijirudie," alisema.

Aidha, alisema Shirika lisilo la kiserikali la Rafiki Wildilife Foundation kwa kushirikiana na Wakala wa Huduma za Misitu (TFS), limetoa miche ya miti 5,000 ili kupandwa kwenye kituo cha Swagaswaga na vijiji vya Kata ya Kwa Mtoro.

Alisema hatua itasaidia kuongeza msitu katika uhifadhi wa mazingira.

Alizitaka taasisi mbalimbali zikiwamo shule na majengo ya nyumba za ibada kutenga maeneo yao kwa ajili ya kuanzisha mradi wa kutengeneza vitalu vya kuotesha miche ya miti, badala kusubiri kuletewa kila mwaka na wadau wa mazingira ambao wamekuwa wakiigawa bure.

Naye Kaimu Kamanda wa Kituo cha Pori la Akiba la Swagaswaga, Ramadhani Abdi, alisema jukumu la kutunza miti lipo kwa kila Mtanzania kwa kushirikiana na serikali.

Abdi alisema kuwa tatizo lililoko kwa baadhi ya wananchi hawapo tayari kuitunza miti na kuipanda, bali wapo wepesi kwa kufyeka misitu na kuchoma mkaa.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Kwa Mtoro, Hussen Chande, aliwataka viongozi wa vijiji na vitongoji kusimamia sheria ndogo ndogo zitakazowabana wanaoharibu mazingira kwa kufyeka na kuchoma misitu.

Aliziomba serikali za vijiji kutumia sheria ndogo ndogo ikiwamo ya kuwalipisha faini ya Sh. 50,000 kwa kila anayepatikana na kosa, ili kujiepusha na uharibifu huo.

# Serikali yashtukia kasi ya usafirishaji haramu wa binadamu ndani ya nchi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Jumanne Sagini, amesema kuna usafirishaji haramu wa binadamu ndani ya nchi ni mkubwa zaidi ikilinganishwa na idadi ya Watanzania wanaosafirishwa kwenda nje ya nchi.

Kutokana na hali hiyo, serikali imezindua mpango kazi wa kitaifa wa kuzuia na kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu ili kukomesha usafirishaji huo.

Sagini aliyasema hayo mwishoni mwa wiki jijini hapo alipokuwa akizindua mpango huo kwenye kikao cha wadau mbalimbali wanaochangia kuzuia na kupambana na biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu.

Alisema kwa upande wa usafirishaji wa ndani ya nchi, wahanga wengi hutumikishwa kufanya kazi za majumbani, kingono, kuchunga ng'ombe, kulima, uvivu, migodini, kufanya biashara ya uchuuzi, utalii wa ngono huku wanaosafirishwa nje ya nchi hususan wanawake wamekuwa wakiokolewa kutoka utumikishwaji wa kingono na kazi za majumbani.

"Nchi ambazo hupelekwa ni pamoja na Thailand, Malaysia, Iraq, Kurdistani, India, Oman na Falme za Kiarabu, wahanga hao wanasema wapo wengine China, Uturuki na Indonesia."

"Waathirika wengine raia wa Tanzania hususan watoto na wenye ulemavu wameokolewa kutoka utumikishwaji wa kuomba mitaani nchini Kenya," alisema.

Sagini alisema serikali inataka kuona nguvu kubwa inaelekezwa katika kutokomeza uhalifu wa usafirishaji haramu wa binadamu kwenye kuelimisha jamii hususani vijijini na kwa kuwashirikisha viongozi wa Serikali za Mitaa.

"Kwa kufanya hivyo tutakuwa tumeokoa watoto, vijana, wasichana na wanawake wengi ambao wangeweza kuwa wahanga wa usafirishaji haramu wa binadamu kama wasingepata elimu husika," alisema.

Aidha, aliwataka wadau kuhakikisha kwamba kila mmoja anapata nakala ya mpango kazi huo kwa ajili ya utekelezaji huku akielekeza wataalamu kupitia mpango kazi walioundaa na kubaini kazi watakazozifanya pamoja na gharama ili kujua fedha zitakazopatikana kutoka serikalini na kutoka kwa wadau.



Kaimu Katibu Tawala wa Wilaya ya Chemba, Rhobi Stephano (kushoto), akimkabidhi Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Kwa Mtoro, Husseni Chande, mche wa mti kwa niaba ya viongozi wa vijiji vilivyoko kata hiyo, iliyotolewa na Asasi isiyo ya kiserikali ya Rafiki Wildilife Foundation kwa kushirikiana na TFS. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# TAKUKURU yashauri wananchi kufuatilia miradi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Dodoma imewataka wananchi kufuatilia kwa karibu miradi ya maendeleo iliyoko katika maeneo yao ili iwanufaishe kiuchumi.

Mkuu wa TAKUKURU mkoani humo, Sosthenes Kibwengo, aliyasema hayo jana kwenye kampeni ya Ulipo Twaja inayowafuata wananchi katika maeneo ya kazi kwa lengo la kutoa elimu ya kujikinga na rushwa jijini hapo.

Kibwengo alisema wananchi wanawajibu wa kuhoji matumizi ya fedha za miradi ikiwamo kutoa taarifa kwa viongozi pindi wanapoona kuna hali isiyoeleweka katika uendeshaji wa miradi ya serikali na kuhakikisha fedha za miradi hiyo zinatumika ipasavyo.

"Wananchi hawapaswi kusubiri miradi iharibike na kuishia kulaumu, isipokuwa wanatakiwa kutoa taarifa kwa viongozi husika ili irekebishwe kwa ajili ya kuisaidia jamii," alisema Kibwengo.

Hata hivyo, alisema jamii inapaswa kujua wajibu wa kuzuia rushwa si wa taasisi pekee, bali ni jukumu la kila mmoja kutoa ushirikiano pale anapoona katika miradi hiyo ya serikali inayotekelezwa na makandarasi ina viashiria vya rushwa ili hatua za kisheria zichukuliwe.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan anasisitiza umuhimu wa kuzuia ubadhirifu wa mali ya umma badala ya kusubiri zifujwe ndipo uchunguzi ufanyike.

Alifafanua kuwa serikali inawekeza fedha nyingi katika miradi ya maendeleo, hivyo jamii inapaswa kutoa ushirikiano wa kuifuatilia na kuhoji namna inavyotekelezwa kwa sababbu ikikamilika kwa wakati italeta manufaa makubwa kwa jamii inayowazunguka.

Kuhusu kampeni ya Ulipo Twaja, Kibwengo alisema imeonyesha matokeo chanya tangu ianzishwe kutokana na wananchi wameonyesha mwitikio mkubwa katika maeneo ambayo wameshayafikia.

Alisema lengo lao ni kuona wananchi wanapata elimu ya rushwa na kuielewa ambayo itawasaidia kujua haki zao za msingi katika maeneo yao ya kazi.



# Mkutano wa wananchi, maofisa Bonde la Ziwa Nyasa wavunjika

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

MKUTANO kati ya wananchi wa Kijiji cha Ikama Kata ya Itagata wilayani Rungwe mkoani Mbeya na Maofisa wa Bonde la Maji la Ziwa Nyasa, umevunjika, baada ya pande hizo mbili kushindwa kuelewana.

Mkutano huo uliandaliwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Kijiji cha Ikama na maofisa wa Bonde la Ziwa Nyasa kwa ajili ya kutoa elimu ya uhifadhi wa chanzo cha maji cha Mto Mbaka kwa wakulima wa Kitongoji cha Mbaka Juu na Nditu.

Mkutano huo uliandaliwa mwishoni mwa wiki ikiwa ni wiki moja baada ya wakulima wa vitongoji hivyo kulalamikia Bodi ya Maji ya Bonde hilo kuvamia mashamba yao na kuweka alama za mipaka zinazoashiria kuwa hawatakiwi kufanya shughuli za kilimo kwenye mashamba hayo yenye ukubwa wa Hekta 57.2 (ekari 143).

Wananchi walifika mapema katika eneo la mkutano wakawa wanawasubiri maofisa wa Bonde ili wawasikilize, lakini baada ya maofisa hao kufika iliibuka hali ya kutoelewana baada ya maofisa hao wa bonde kutotaka waandishi wa habari wawepo.

Mkuu wa msafara wa maofisa hao aliyejitambulisha kwa jina moja la Elice, aliwaita waandishi wa habari waliokuwapo eneo la tukio na kuwataka waondoke eneo la mkutano akidai kuwa yeye ndiye mwenye mkutano na hakualika kundi hilo.

Elice alisema anapokuwa anahitaji waandishi wa habari huwa anawaalika lakini kwenye mkutano huo na wananchi hakuwa na uhitaji wa waandishi hao.

"Kwanza mnatakiwa mnapokuja kufanya kazi za habari mnatakiwa kuripoti kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ili yeye ndiye awaruhusu kufanya kazi hii, kwa sasa nawaambia kwamba kwenye mkutano wangu siwahitaji," alisema Elice.

Baada ya mazungumzo na waandishi wa habari, ofisa huyo pamoja na wasaidizi wake aliokuwa ameongozana nao walirejea eneo la mkutano, lakini wananchi wakagoma kuwasikiliza bila uwapo wa waandishi wa habari.

Wananchi hao waliondoka na kuwatelekeza maofisa hao ambao nao walijadiliana kwa muda usiozidi dakika 10 na kisha wakaondoka na magari yao.

Baadhi ya wananchi hao walisema pamoja na maofisa hao kuwafukuza waandishi, lakini walionyesha dharau kwao kwa kuwatamkia maneno ambayo yalikuwa ya kukera.

Mmoja wa wananchi hao, Asumwisye Mwaipopo, alisema maofisa hao waliwaambia kuwa wasingefanya mkutano huo kutokana na idadi ya watu waliohudhuria kuwa ndogo.

Alisema awali wakati unajengwa mradi wa maji wa Masoko Group na wa kupeleka maji Tukuyu Mjini waliahidiwa kuwa na wao wangenufaika, lakini mpaka sasa hawajawahi nufaika zaidi ya kuanza kuumizwa kwa kuporwa mashamba.

"Sisi tumekuwa tukilima kwa kufuata sheria ya vyanzo vya maji kwa kuacha mita 60 ambazo tulielimishwa tukaelewa na tukashiriki hata kupanda miti rafiki kwenye vyanzo, sasa tunashangaa wao wanakuja kupima mpaka zaidi ya mita 6,000," alisema Mwaipopo.

Mwenyekiti wa wananchi wenye mashamba hayo, Brown Mwangake, alisema maofisa hao wanasababisha mgogoro ambao hauna sababu kutokana na kuweka alama kwenye mashamba yao bila kuwashirikisha hata viongozi wa vijiji.

Aliiomba serikali iingilie kati ili wajue hatima yao kwa maelezo kuwa mashamba hayo ndiyo wanayategemea kwa ajili ya uendeshaji wa maisha ya familia zao.



Malori yakiwa yamekwama katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi mkoani Mbeya mwishoni mwa wiki, baada ya mojawapo kushindwa kushuka mteremko wa Mlima Mbalizi na kusababisha foleni. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Daraja lililoua 5 laanza kujengwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI kupitia Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA), imeanza ujenzi wa daraja linalounganisha kata za Mwasanga, Tembela na Mwakibete jijini Mbeya ambalo lilibomoka mwaka 2019 na kusababisha vifo vya watu watano.

Daraja hilo limeanza kujengwa wiki mbili baada ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, kutembelea eneo hilo na kusema serikali imetenga Sh. bilioni 1.4 kwa ajili ya ujenzi huo.

Waziri Bashungwa aliagiza TARURA kuanza ujenzi wa daraja hilo Machi 1, mwaka huu, ili likamilike haraka na wananchi waanze kutumia ili kuondoa kero ambayo inawakabili kwa sasa.

Daraja hilo lilianza kujengwa jana ambapo mkandarasi alianza kwa kuliondoa daraja la zamani na kuondoa udongo wa juu ili shughuli ya ujenzi.

Meneja wa TARURA Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Wilson Charles, alisema ujenzi wa mradi huo utakamilika katika kipindi cha miezi sita pekee na hivyo akawataka wananchi kutoa ushirikiano kwa mkandarasi.

"Fedha kwa ajili ya mradi huu tulishaletewa na Waziri wa TAMISEMI na hivyo kilichobaki sasa ni ujenzi ambao tayari umeshaanza kama mnavyoona, tutasimamia ili kuhakikisha unakamilika ndani ya muda uliopangwa," alisema Mhandisi Charles.

# Wananchi Mbeya walia ubovu wa barabara

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANANCHI wa Kata ya Shizuvi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wameomba serikali kuwaboreshea barabara inayounganisha kata hiyo na Kata ya Ilembo ili kuwarahisishia mawasiliano hasa kipindi hiki cha mvua ambacho walisema haipitiki kabisa.

Walitoa kilio hicho wakati wa mkutano wa hadhara ulioitishwa na Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua, na kufanyika katika Kijiji cha Inyala-Ilembo ambapo walisema barabara hiyo ni kero yao ya muda mrefu na inakwamisha maendeleo.

Mmoja wa wananchi hao, Mariam Mwamahonje, alisema wanawake ndio wanaopata shida zaidi ya barabara hiyo hasa wanapotakiwa kwenda kujifungulia kwenye Kituo cha Afya cha Ilembo. Alisema katika kijiji chao ipo zahanati, lakini wakati mwingine huwa inashindikana kujifungulia hapo na wanapewa rufani ya kwenda kujifungulia Ilembo ambako alisema ni mbali na barabara yao imekuwa ikiwaongezea matatizo.

Alisema wanapopewa rufani ya kwenda kujifungulia Ilembo huwa wanasafirishwa kwa pikipiki, jambo ambalo alisema kutokana na ubovu wa barabara hiyo matatizo huwa yanaongezeka zaidi na wakati mwingine huwa wanaumia.

Alisema huwa wanaanguka na pikipiki na hivyo kufika kituo cha afya wakiwa wamechoka na hivyo kujifungua kwa shida kutokana na uchovu unaosababishwa na ubovu wa barabara.

"Wakati mwingine mwanamke anajifungua kabla ya wakati kutokana na kurushwarushwa na pikipiki, wengine wanapata shida kujifungua kwa sababu wanakuwa wamechoka, sasa tunaomba utufikishie salamu kwa Rais wetu Samia atuonee huruma wanawake wenzake," alisema Mariam. Naye Sophia Shila, alisema kutokana na ubovu wa barabara hiyo wanatumia gharama kubwa kusafirisha bidhaa hali ambayo inayosababisha hata bei kuongezeka.

Jimbo la Mbeya Vijijini, Oran Njeza, aliiomba serikali kuipandisha hadhi barabara hiyo ili badala ya kusimamiwa na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) isimamiwe na Wakala wa Bararara nchini (TANROADS).

Alisema barabara hiyo ni muhimu kwa sababu inaunganisha Kata mbili za Wilaya ya Ileje na tatu za Wilaya ya Mbeya na hivyo ni muhimu kwa maendeleo ya pande hizo mbili. "Hili eneo ni miongoni mwa maeneo muhimu sana kiuchumi, wananchi wa huku ni wakulima wazuri sana, lakini tatizo hili la barabara linawaathiri sana hivyo Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya tunaomba ipandishwe hadhi," alisema Njeza.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Chuachua aliahidi kushughulikia tatizo hilo kwa kuwaagiza TARURA kuikarabati ili iwe inapitika mwaka mzima badala ya kupitika kipindi cha kiangazi pekee.

Alisema mbali na barabara hiyo, pia zipo barabara zingine za wilaya hiyo ambazo miundombinu yake sio mizuri hasa kipindi hiki cha mvua na hivyo akasisitiza kuwa atawaagiza TARURA kuziweka kwenye vipaumbele vya ujenzi.





# Majaliwa ataka watendaji sensa kuwa wawazi

**Na Mwandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Kamati ya Kitaifa ya Sensa ya Watu na Makazi, Kassim Majaliwa, amewataka watendaji wanaosimamia kuwa wawazi katika majukumu yao ili kuendana na azma ya serikali zote mbili kwa kuwaletea maendeleo wananchi wake.

Majaliwa ambaye ni Waziri Mkuu alitoa agizo hilo alipokuwa akiendesha kikao cha nne cha kamati hiyo kilichofanyika mjini hapo.

Alisema ni vyema kwa matumizi ya vifaa vitakavyotumika kwa ajili ya Sensa ya Watu na Makazi yafanywe kwa kufuata utaratibu ili kutumia fedha kwa mujibu wa sheria za ununuzi zilizoko nchini.

Naye Mwenyekiti Mwenza wa Kamati ya Kitaifa ya Sensa ya Watu na Makazi, Hemed Suleiman Abdulla, ambaye ni Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, amezitaka wizara husika kuacha muhali katika kutoa nafasi za ajira. Alisema ni vyema kuzingatia vigezo vinavyohitajika kupatikana watumishi hao watakaoendesha sensa hiyo.

Alisema serikali haitoridhia kuona baadhi ya watumishi wake wanavuruga sensa hiyo kwa maslahi yao binafsi na kwamba hatua za kisheria zitachukuliwa kwa yeyote atakayevuruga.

Hata hivyo, Hemed alisema serikali ina matumaini makubwa kwa sensa na kuwa ni vyema kila mmoja akahakikisha anawajibika ipasavyo ili kukamilika kwa maslahi ya taifa.

Kwa upande wao Makamisaa wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 walisema makarani watakaotumika kusimamia watachukuliwa kwa mujibu wa maeneo yao ya makazi ili kuhakikisha inakamilika kwa urahisi na kwa wakati uliopangwa.

## Watakaobainika kufuja fedha za miradi kukiona

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema itachukua hatua kali za kinidhamu kwa watendaji watakaobainika kufuja fedha za miradi ya maendeleo katika sekta ya maji, elimu na ujenzi wa hospitali 10 za wilaya ya Unguja na Pemba.

Hayo yalisemwa na Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdalla, wakati akizungumza na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi katika kikao cha baraza hilo na kuwataka viongozi hao kufuatilia miradi hiyo inayotekelezwa katika majimbo yao.

Alisema serikali imetenga fedha za janga la UVIKO-19 kwa malengo muhimu ya kuimarisha sekta ya afya, elimu, miundombinu pamoja na ujenzi wa masoko kwa ajili ya wajasiriamali wanawake.

Kadhalika, alisema Sh. bilioni 230 ni fedha nyingi ambazo zikitumika vizuri kwa malengo yaliyokusudiwa zitasaidia kuharakisha maendeleo ya wananchi.

Aliwataka watendaji ikiwamo wajumbe wa Baraza la Wawakilishi pamoja na wabunge kufuatilia kwa karibu sana maendeleo ya fedha hizo kuona zinatumika vizuri kwa malengo yaliyokusudiwa ambayo ikifanikiwa itawapunguzia kwa kiasi kikubwa majukumu.

Alisema kuwa serikali imetenga Sh. bilioni 68.500 kwa ajili ya sekta ya afya ikiwamo ujenzi wa hospitali 10 za wilaya ya Unguja na Pemba pamoja na hospitali moja ya mkoa itakayojengwa Lumumba Mjini Unguja.

Pia katika fedha hizo Sh. bilioni 22 zitatumika kwa ajili ya ujenzi wa hospitali 10 za wilaya ya Unguja na Pemba huku Sh. bilioni 14 zitatumika kwa kujenga hospitali moja kubwa ya Lumumba Unguja.

Kwa upande wa sekta ya elimu alisema, serikali imetenga Sh. bilioni 68.500 ikiwamo shule za mjumuisho pamoja na za ghorofa zitakazopunguza msongamano wa wanafunzi huku Sh. bilioni 16.45 zitatumika ujenzi wa madarasa 706 katika wilaya zote.

Aliwapongeza wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kupitisha muswada wa kuanzishwa kwa wakala wa uwezeshaji wananchi kiuchumi ambao utatumika moja kwa moja katika kusimamia fedha za wajasiriamali kuwafikia walengwa.



Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Zubeir Ali Maulid, akikagua bidhaa za viatu na nguo zinazotengenezwa katika kiwanda cha Zanzibar Quality Tailoring Limited kilichoko chini ya Idara Maalum za SMZ, alipotembelea maonyesho hayo viwanja vya Baraza la Wawakilishi Chukwani. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Wawakilishi wapitisha muswada wa kuanzisha wakala uwezeshaji wananchi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi wamepitisha muswada wa kuanzishwa kwa wakala wa uwezeshaji wananchi kiuchumi ambao umelenga kusimamia mwenendo wa fedha za wajasiriamali kuona zinatumika vizuri kuwakomboa wananchi kiuchumi na hali ngumu ya maisha.

Akijibu hoja za Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliochangia muswada huo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga, alisema serikali imeleta muswada huo kwa hati ya dharura kwa lengo la kuona fedha za uwezeshaji wananchi kiuchumi zinatumika vizuri kwa maslahi ya taifa.

Alisema kwa muda mrefu serikali imekuwa ikitoa fedha hizo kwa nyakati tofauti, lakini malalamiko mbalimbali yameibuka ikiwamo walengwa kutofikiwa kikamilifu.

Alisema kuwa kuwapo kwa wakala wa uwezeshaji kwa kiasi kikubwa atakuwa na majukumu ya kuratibu fedha za uwezeshaji pamoja na kutoa mafunzo kwa walengwa ya matumizi sahihi ya fedha hizo.

Alisema kwa muda mrefu serikali imefanikiwa kutoa fedha kwa wajasiriamali katika mifuko ya Jakaya Kikwete (JK) na Amani Karume (AK), lakini kwa bahati mbaya hazikuratibiwa vizuri na matokeo yake malengo yaliyowekwa hayakufikiwa kikamilifu.

Vile vile, alisema serikali imetenga Sh. bilioni 47.330 kwa ajili ya uwezeshaji wajasiriamali mbalimbali Unguja na Pemba ambazo zitaleta mabadiliko makubwa na kubadilisha maisha ya wananchi kuwa bora. Alisema Sh. bilioni 28.84 zimetengwa kwa ajili ya uchumi wa buluu ikiwamo kilimo cha mwani na wakulima watapatiwa boti za kufika katika maeneo ya kilimo ambacho ni kina kirefu cha maji.

"Mheshimiwa Spika nataka niwajulishe Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba fedha za wajasiriamali tumepanga kikamilifu kuzitumia vizuri ndiyo maana serikali imeamua kuleta mswada huu utakaoratibu matumizi ya fedha hizo," alisema.

Baadhi ya wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wamepongeza muswada huo ambao utakuwa mwarobaini wa kuyapatia ufumbuzi matatizo yanayowakabili wajasiriamali wanawake katika harakati zao za kujikomboa.

Mwakilishi wa Jimbo la Mahonda, Asha Abdalla Mussa, alisema juhudi kubwa zinafanywa katika kuwawezesha wanawake kujikomboa kiuchumi, lakini tatizo hakuna usimamizi wa fedha hizo.

Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wamepitisha muswada huo wa kuanzisha wakala wa uwezeshaji wananchi kiuchumi kwa ajili ya kuwapo kwa mfumo mmoja utakaofanya kazi zote ikiwamo kubuni na kutafuta fedha.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

## KUPOTEA KWA CHETI CHA KIDATO CHA NNE



**ELIAZALI SHELOME LUKINISHA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0385-0112** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia shule ya secondari ya ujiji mwaka 2014. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/OST/RB/94773/2022**

## KUPOTEA KWA CHETI CHA KIDATO CHA NNE



**VICTOR BUBERWA FELIX** anatangaza kupotea kwa cheti chake cha kidato cha nne chenye usajili namba **S.2710-0029** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia shule ya sekondari YA RUZINGA mwaka 2017. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: **MWA/NY/RB/478749/2021**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**MOHAMED ENTERPRISES** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya BOXER yenye usajili namba **MC 334 CLP.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**ARU/ARU/RB/94808/2022**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA MAHALI DODOMA**

**MAOMBI MADOGO NA. 112 YA 2022**

**BAINA YA**

**METHEW SILAYO......................MKAZA HUKUMU/MUOMBAJI**

**DHIDI YA**

**CONSOLATA DAUDI ......... MKAZIWA HUKUMU/MJIBU MAOMBI**

**KWA: CONSOLATA DAUDI**
**POPOTE ULIPO**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya maombi inapatikana katika Baraza hili.

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 15/03/2022 saa 3:00 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.

**ANAGALIZO:-** kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likidhibitisha kuwa umepokea hayi ya Wito, Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na lakiri /Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 03 ya m[illegible]

MWENYEKITI,
Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya,
Dodoma.

Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KITAIFA

## Fedha za UVIKO kuwanoa wadau wa utalii

Na Richard Makore, MWANZA

SERIKALI imelenga kuongeza idadi ya watalii nchini kutoka 620,000 katika kipindi cha ugonjwa wa UVIKO-19 na kufikia milioni tano ifikapo mwaka 2025.

Idadi hiyo inatarajiwa kuongezeka kupitia mipango mbalimbali inayofanywa na serikali ikiwamo utoaji wa elimu kwa wadau wa utalii.

Akizungumza katika semina ya siku tano ya wadau wa utalii, Mtendaji Mkuu wa Chuo cha Taifa cha Utalii, Dk. Shogo Mlozi, alisema mpango wa serikali ni kuhakikisha ifikapo mwaka 2025 watalii wanafikia milioni tano.

"Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), inaitaka serikali kuongeza idadi ya watalii hadi kufikia milioni tano ili kuhakikisha pato la taifa linaongezeka kupitia sekta ya utalii nchini," alisema.

Dk. Mlozi alisema sekta ya utalii iliathiriwa na UVIKO-19 na kwamba serikali kupitia chuo chake inafanya jitihada mbalimbali ikiwamo kuandaa semina kwa wadau zitakazosaidia kuongeza watalii nchini.

Alisema serikali imewapatia fedha za UVIKO-19 ili kutoa semina kwa wadau wa utalii katika mikoa minane nchini na kwamba hatua hiyo inalenga kuwajengea uwezo wa mafunzo ili kuwawezesha kupokea watalii na kuwakarimu.

Alitaja mikoa iliyopata mafunzo hayo kuwa ni pamoja na Iringa, Njombe, Mwanza, Mara, Ruvuma, Mbeya, Mtwara na Lindi.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Magu, Salum Kali, akifungua semina hiyo kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel alisema, sekta ya utalii ni muhimu katika kukuza pato la taifa.

Aliwaasa wadau mbalimbali Kanda ya Ziwa kufungua kampuni za utalii ili kupokea watalii na kuwatembeza katika vivutio mbalimbali vilivyopo eneo hilo.

Alisema Mkoa wa Mwanza ni miongoni mwa mikoa Kanda ya Ziwa, ambao una vivutio vingi likiwamo Ziwa Victoria, Hifadhi ya Saanane, ngoma za asili, mawe mazuri pamoja na kuona watu wanavyocheza na nyoka.

"Yaani hapa Mwanza mtalii anaweza kutembelea maeneo mbalimbali ya ufukwe wa ziwa, mawe, sehemu za ngoma za asili, hifadhi nzuri ya Saanane kwa ajili ya kujionea utalii," alisema Kali.

Katika semina hiyo ya siku tano wadau 156 wa utalii watapatiwa mafunzo ili kuwaandaa kupokea watalii na namna ya kuutangaza.

# Wakili ajitoa kesi ya kina Sabaya

Na Waandishi Wetu, ARUSHA

WAKILI Fridolin Bwemelo wa mshtakiwa wa tatu katika kesi ya uhujumu uchumi inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, amejitoa kumtetea mteja wake, Watson Mwahomange (27), kwa madai kwamba wameshindwa kuelewana.

Wakili huyo alitoa madai hayo jana mbele ya Hakimu wa Mahakama ya Hakimu Mkazi, Dk. Patricia Kisinda, katika kesi ya uhujumu uchumi inayomkabili Sabaya na wenzake sita.

Washtakiwa wengine, katika kesi hiyo ni Lengai Ole Sabaya, Silvester Nyegu (26), Enock Togolani (41), John Odemba, Jackson Macha (29) na Nathan Msuya (31) na wanakabiliwa na mashtaka matano likiwamo la matumizi mabaya ya madaraka, kuongoza genge la uhalifu, kujihusisha na vitendo vya rushwa na utakatishaji wa fedha.

Akizungumza mahakamani wakili huyo, alidai kwamba amejitoa kumwakilisha mshatakiwa huyo kwa kuwa amekuwa akienda kinyume cha maelekezo anayopewa, hivyo amejitoa ili kulinda kiapo alichotoa mahakamani.

"Mheshimiwa hakimu, nimeamua kujitoa kumwakilisha mshtakiwa wa tatu kwa kuwa amekuwa anakwenda kinyume cha maelekezo ya wakili anayemtetea," alidai.

Vilevile, alidai kwamba ataendelea kumwakilisha mshtakiwa wa nne katika kesi hiyo, John Odemba hadi kukamilisha kutoa ushahidi wake mahakamani.

Baada ya kuwasilisha hoja hiyo, mahakamani, akianza kutoa ushahidi mshtakiwa wa pili katika shauri hilo, Enock Togolani, alidai kwamba hamfahamu wala hakuwahi kuwa mlinzi wa Sabaya.

Kadhalika, alidai hakuwahi kufika katika karakana ya mfanyabiashara Francis Mroso iliyoko Mbauda jijini Arusha.

Alidai hakuwahi kuhusika kumlazimisha Mroso kutoa Sh. milioni 90 kama ilivyodaiwa mahakamani na mashahidi wakati wakitoa ushahidi.

Katika kesi hiyo, shtaka la kwanza ni la kuongoza genge la uhalifu kinyume na Sheria ya Uhujumu Uchumi kifungu cha 57(1) na 60(2) na linawakabili washtakiwa wote.

Shtaka la pili ni la kujihusisha na vitendo vya rushwa na linamkabili mshtakiwa wa kwanza peke yake, na ni kinyume cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kifungu cha 15(1B,2) sura ya 329 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2019.

Shtaka la tatu ni la kujihusisha na vitendo vya rushwa, linalomkabili mshtakiwa wa kwanza peke yake, kinyume cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kifungu cha 15(1B,2) sura ya 329 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2019.

Shtaka la nne ni la matumizi mabaya ya madaraka, linalomkabili Sabaya peke yake, kinyume na kifungu cha 31 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa sura ya 329 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2019.

Shtaka la tano ni la utakatishaji wa fedha na linalowakabili washtakiwa wote saba, ni kinyume na kifungu 12(D),13(1A), cha Sheria ya Utakatishaji Fedha sura ya 423 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2019.

**Imeandikwa na Tumaini Mafie na Allan Isaack, Arusha**



Mwanachama wa Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni jijini Dar es Salaam, Juma Rashid, akipanga mkaa unaotengenezwa na kituo hicho kwa kutumia takataka, maboksi, vifuu vya nazi, majani na vumbi la mbao kwa ajili ya kutunza mazingira juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wafungwa miaka 30 jela, viboko 12 kwa unyang'anyi

Na Joctan Ngelly, GEITA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Geita imewahukumu watu watatu kutumikia kifungo cha miaka 30 jela na viboko 12 kwa kosa la unyang'anyi wa kutumia silaha. Watu hao walishtakiwa kwa kosa la kuvamia nyumba kwa mapanga na marungu na kuiba vitu mbalimbali vyenye thamani ya Sh. 2,930,000 mali ya Mateja Mugeta.

Waliohukumiwa ni Oscar Ibrahim (24), Issaya Ibrahim (18) na Mkina Baraka (20), wote kwa pamoja ni wakazi wa Shilabela, Wilaya ya Geita.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa mahakama hiyo, Samwel Maweda baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha kosa hilo pasipokuacha shaka yoyote.

Hakimu Maweda alisema mahakama hiyo inatoa adhabu kali dhidi ya washtakiwa hao ili iwe fundisho kwao na kwa vijana wengine wenye tabia ya wizi.

Alisema upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali Winfrida Mpiwa, ulipeleka mashahidi sita na vielelezo mbalimbli ambavyo vilithibitisha kuwa washtakiwa hao walitenda kosa hilo.

Alisema upande wa utetezi ulikuwa ukiongozwa na Wakili wa kujitegemea Ribelatus John.

Hakimu Maweda alisema ameangalia ushahidi wa pande zote na kugundua kuwa upande wa mashtaka umethibitisha kosa pasipokuacha shaka yoyote na kuwatia hatiani washtakiwa wote kwa pamoja kwa kosa walilolshtakiwa.

Washtakiwa wote kwa pamoja wakiongozwa na wakili John waliomba mahakama hiyo iwapunguzie adhabu kwa kuwa wana familia inayo wategemea.

Upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali Winfrida Mpiwa, uliomba mahakama hiyo itoe adhabu kwa mujibu wa sheria.

Hakimu Maweda alisema kitendo walichokifanya washtakiwa wote kwa pamoja kwa kuvamia nyumba na mapanga na marungu na kuiba vitu mbalimbali ni kitendo cha kikatili.

Alisema upande wowote ambao haujaridhika na uamuzi huo rufaa ipo wazi.

Awali, akisoma hati ya mashtaka wakili Mpiwa alidai kuwa Machi 2020 majira ya usiku huko Bomani, Mkoa wa Geita washtakiwa wote kwa pamoja walivamia nyumba na mapanga na marungu na kuiba vitu mbalimbali vyenye thamani ya Sh. 2,930,000 mali ya Mateja Mugeta kinyume cha sheria.

# DK. NDUMBARO ATETA NA AJAX KUTANGAZA VIVUTIO VYA UTALII

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, amefanya mazungumzo na uongozi wa Klabu ya Soka ya Ajax ya Uholanzi, ili itangaze vivutio vya utalii vya Tanzania kupitia matangazo ya jezi na mbao za matangazo (billboards) katika uwanja wao.

Waziri Ndumbaro, ambaye amefanya ziara ya kikazi nchini Uholanzi kwa lengo la kutafuta fursa za kutangaza vivutio vya utalii nchini humo, alibainisha hayo jana alipokutana na kufanya mazungumzo na viongozi wa klabu hiyo wakiongozwa na Ofisa Mkuu wa Uwanja, Tanja Dik na Mkurugenzi wa Fedha wa timu hiyo, Han Mouton.

Katika mazungumzo yao, Dk. Ndumbaro aliwasilisha nia ya Tanzania kushirikiana na Klabu ya Ajax katika kutangaza vivutio vya utalii vilivyoko nchini kupitia matangazo kwenye jezi na mbao za matangazo zilizoko katika uwanja wa klabu hiyo.

"Mazungumzo yetu yameenda vizuri na viongozi hao wamepokea pendekezo na ombi letu na kuahidi kulifikisha kwenye idara husika ya biashara pia kuendeleza mawasiliano na ubalozi wetu ulioko hapa kuangalia namna ya kutekeleza nia hii," alisema Dk. Ndumbaro.

**Katika hatua nyingine, Dk. Ndumbaro alitembelea na kufanya mazungumzo na uongozi wa Klabu kubwa ya Gofu nchini Uholanzi ya GC BurgGolf Westerpark, Zoetermeer.**

Katika mazungumzo yake na Meneja Mauzo na Matukio, Eline Dujardin na Mkufunzi katika klabu hiyo, Ronald Mos, Dk. Ndumbaro aliwasilisha pendekezo la Tanzania kushirikiana na klabu hiyo katika kuandaa tamasha la gofu litakalofahamika kwa jina la "Mt. Kilimanjaro Open".

Pendekezo hilo lilipokelewa vizuri na viongozi wa klabu hiyo na kuahidi kuwasiliana zaidi kupitia ubalozi ili kuangalia namna bora ya kulitekeleza. Aidha, Waziri Ndumbaro pia alifanya mazungumzo na Balozi wa Tanzania nchini Uholanzi, Irene F. M. Kasyanju pamoja na watumishi walioko ubalozini hapo.




Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, akiwa na Balozi wa Tanzania nchini Uholanzi, Irene Kasyanju, wakati wakizungumza na Meneja Masoko wa Klabu ya Ajax , Ted Robinson baada ya kutembelea duka la jezi za Klabu ya Ajax nchini humo mwishoni mwa wiki. **MPIGAPICHA WETU**

## Tanga City Marathon kutimua vumbi Machi 27

**Na Cheji Bakari,** TANGA

MASHINDANO ya riadha Mkoa wa Tanga ya awamu ya sita maarufu kwa jila la 'Tanga City Marathon Season 6', yanatarajiwa kutimua vumbi Machi 27, mwaka huu, mkoani hapo.

Mratibu Mkuu wa mashindano hayo, Ali Mang'oro, amesema hadi sasa jumla ya washiriki 150 kutoka mikoa mbalimbali tayari wamejiandikisha kushiriki na kwamba yatakuwa ya mbio za kilometa 21, 10 na tano kwa wanaume na wanawake.

"Hadi sasa washiriki zaidi ya 150 kutoka mikoa ya Tanga, Dar es Salaam, Iringa, Kilimanjaro, Arusha na Manyara wameshajiandikisha kushiriki mashindano hayo na nafasi bado zipo," alisema Mang'oro.

Aliongeza: " Hadi sasa zikiwa zimebaki takriban wiki tatu, bado hatujapata wadhamini, tunafanya maandalizi kwa fedha zetu wenyewe, tumepeleka miswada yetu kwa wadhamini mbalimbali bado hatujapata majibu, hivyo tunaomba wadhamini kujitokeza kuudhamini mchezo huu."

Aidha, alisema katika mashindano hayo yaliyoasisiwa mwaka 2017 na mdau wa riadha ambaye ni mkazi wa Mkoa wa Tanga, Juma Mwajasho, ili kuleta mapinduzi ya michezo kutoka kupenda zaidi mchezo wa soka hadi riadha, ya mwaka huu mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Adam Malima.

Alisema lengo kubwa la mashindano hayo ni kuibua vipaji vya mchezo huo kwa vijana mkoani Tanga ambapo mchezo wa riadha haukupewa kipaumbele, hivyo kuufanya kuwa fursa ya ajira badala ya kutegemea soka pekee.

# *Mayele ampa mtoto bao, Mpole ataka Kiatu*

**Adam Fungamwango na Shufaa Lyimo**

WAKATI Fiston Mayele akifunga bao kwenye mechi ya Ligi Kuu juzi kati ya timu hiyo na Geita Gold na kulitoa zawadi kwa mtoto wake wa kwanza ambaye anasherehekea siku yake ya kuzaliwa leo Machi 8, straika George Mpole amesema kuwa pamoja na kukosa mabao mengi kwenye mechi hiyo, bado anataka kuwa mfungaji bora msimu huu.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti baada ya mechi kati ya timu hizo, Yanga ikishinda bao 1-0, mastraika hao kila mmoja aliongelea mbio za kuwania Kiatu cha Dhahabu, Mpole mwenye mabao manane akijinasibu kuwa atakitwaa, huku Mayele ambaye amefikisha bao la 10, akidai bado mchuano ni mgumu.

"Nashukuru sana kufunga bao hili, nampa mtoto wangu wa kwanza, hili ni kwa ajili yake, nilimpigia simu nikamwambia nitafunga goli la zawadi kwa ajili yake, na kweli nimefunga, nimefurahi sana," alisema Mayele ambaye sasa anachuana kileleni na Relliants Lusajo wa Namungo mwenye mabao kama hayo, wote wakiwa wanaongoza.

Kuhusu ufungaji bora, Mayele alisema pamoja na kwamba yuko juu, lakini akakiri kuwa upinzani ni mkali na anaochuana nao wote ni wazuri.

"Upinzani ni mkubwa sana, ninaokimbizana nao ni mastraika wazuri. Mpole anacheza vizuri, Lusajo naye ni straika mzuri na nafasi ya ufungaji bado ni ngumu siwezi kusema lolote kwa sasa, ila nashukuru nimefunga bao la 10," alisema straika huyo raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo.

Mpole yeye alisema kukosa mabao mengi kwenye mechi ya Yanga haimkatishi tamaa, kwani kipa wa Yanga Djigui Diarra ndiye aliyemnyima mabao.

"Nilipata nafasi, kwa straika lazima upate nafasi, lakini kipa alizicheza ambazo tulitakiwa tufunge, zingine zilikwenda nje, ni kawaida tu kwenye mpira," alisema na kuongeza.

"Kwangu mimi nitaendelea kupambana, najua mechi zipo nyingi na nafasi nyingi nitapata, nitakuwa na umakini, nitafunga, Mungu akijalia hicho Kiatu cha Dhahabu nitakichukua tu," alisema.

TANGAZO


# KONGAMANO LA UCHUMI WA BULUU NA WANAWAKE ZANZIBAR




RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt.Hussein Ali Mwinyi, akihutubia katika hafla ya ufunguzi wa kongamano la wanawake wajasiriamali lililoandaliwa na Benki ya Biashara Tanzania (TCB) Jumamosi wikiendi iliyopita kama sehemu ya mkakati wake wa kuwashirikia akinamama katika ujenzi wa taifa na kuwajenga kibiashara kupitia Uchumi wa Buluu.



RAIS wa Zanzibar, Dk.Hussein Mwinyi, akikabidhiwa Kadi ya Akaunti yake ya Benki ya Biashara Tanzania (TCB) na Afisa Mtendaji Mkuu wa benki hiyo, Bw. Sabasaba Moshingi baada ya kufunguliwa kwa Kongamano wa Wanawake Zanzibar. Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ni moja wa wanahisa wa TCB ikiwa na umuliki wa asilimia 3 kwenye taasisi hiyo kongwe ya fedha nchini ailiyoangziashwa mwaka 1925.




Dk.Hussein Mwinyi akimkabidhi hundi yanye thamani ya TZS milioni 15??? kiongozi wa Kikundi cha Wajasiriamali cha Chaza Mpya wakati wa ufunguzi wa Kongamano la Wanawake Zanzibar. Katikati ni Mke wa Dkt Mwinyi, Bi Marium Mwinyi, ambaye ushiriki wake kwenye kongamano hilo liliandaliwa na Benki ya TCB uliwatia hamasa wajasiriamali wanawake waliohudhiria shughuli hiyo iliyofana na kuwaelimisha akinamama mambo mengi ya kibiashara na kiuzalishaji.



Miongoni mwa washiriki wa Kongamano la Wanawake na Biashara la Zanzibar lililojikita zaidi kuchambua ushiriki wa akinamama kwenye Uchumi wa Buluu kwa ajili ya maendeleo endelevu walikuwa ni wakurugenzi wa TCB ambao baadhi yao walitoa mada kuhusu fursa lukuki za kihuduma ilizonazo benki hiyo za kuwawezesha wanawake kiuchumi na kibiashara.




RAIS Dk.Hussein Ali Mwinyi akikabidhiwa zawadi maalum ya picha ya kuchora na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Benki ya Biashara Tanzania (TCB), Dkt Edmund Mndolwa, baada ya ufunguzi wa Kongamano la Wanawake Zanzibar Jumamos wiki iliyopita. Wanaofurahia picha hiyo ni pamoja na Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii Wazee Jinsia na Watoto Zanzibar, Bw Nassor Ahmed Mazrui (kulia kwa Rais), Afisa Mtendaji Mkuu wa TCB, Bw. Sabasaba Moshingi (wa pili kushoto) na Katibu wa Baraza la Mapinduzi Mhandisi Zena Ahmed Said (kushoto).



WASHIRIKI wa Kongamano la Wanawake Zanzibar ambao walikuwa wengi sana ukilinganisha na maudhurio ya makongamano yaliyotangulia ya aina hiyo ya kuwawezesha akinamama kiuchumi yaliyofanyika Dodoma, Mbeya na Mwanza wakimsikiliza Rais Dkt Huessin Mwinyi wakati wa ufunguzi wake Jumamosi kwenye Hoteli ya Golden Tulip Kiembesamaki.

Tanzania Commercial Bank
Growing stronger together

Innovative Banking Solutions for Economic Development

P.O.Box 9300, Dar Es Salaam Email: **Info@tcbbank.co.tz**
Fax: +255 788767683, 658767683
Website: www.tcbbank.co.tz

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 1,013

MECHI KALI
LIVERPOOL
VERSUS
INTER
1 | 1.57
X | 4.31
2 | 5.21

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# XAVI ASEMA BARCA ILISTAHILI BAO ZAIDI

**BARCELONA,** Hispania

XAVI aliachwa amekatishwa tamaa na ushindi wa Barcelona dhidi ya Elche kwani haukutosha na kujikuta akiingia kwenye mzozo na kocha mwenzake.

Barca walilazimika kutoka nyuma na kupata ushindi huo Jumapili, hivyo kuwafanya wafikishe mechi 11 bila kufungwa kwenye Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga.

Fidel aliipa bao Elche dakika ya 44 huku shuti la Frenkie De Jong likiokolewa na golikipa, Edgar Badia.

Bao la kwanza la Ferran Torres kwa Barca liliwarudisha mchezoni, lakini 'Blaugrana' hao walihitaji penalti ya Memphis Depay kuweza kupata ushindi wa mabao 2-1.

Kocha wa Elche, Francisco Rodriguez na straika Pere Milla walionekana kuzozana na Xavi baada ya mchezo huo.

Alipoulizwa nini kilichotokea kwenye mzozo wao, Xavi alijibua: "Hakuna chochote. Usilifanye kuwa jambo muhimu sana. Ni hali ya kawaida tu.

"Bora kuzungumzia kuhusu mechi na hali yake kwa ujumla. Heshima kwa Elche na Francisco."

Aliongeza: "Nafiriki tulistahi mabao zaidi, kwa sababu tulikuwa na kiwango bora zaidi."



## Arteta awasifia Saka, Odegaard

**LONDON,** England

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta, alisifia ubora wa Bukayo Saka na Martin Odegaard baada ya wote kufunga kwenye ushindi wa mabao 3-2 dhidi ya Watford.

Saka na Odegaard walifunga kipindi cha kwanza kabla ya Gabriel Martinelli kufunga la tatu, huku Watford mabao yake yakifungwa na Cucho Hernandez na Moussa Sissoko.

Arsenal, ambao wanapambana kumaliza kwenye nafasi ya nne bora kwa mara ya kwanza tangu mwaka 2016, wameshinda mechi nne mfululizo za Ligi Kuu England.

Saka sasa amechangia mabao 13 kwenye Ligi Kuu msimu huu (mabao nane na asisti tano).

Ingawa Arteta hakufurahishwa na kiwango cha ulinzi cha Arsenal pale kwenye dimba la Vicarage Road, alielezea namna wawili hao walivyotoa mchango mkubwa kwa 'Washikabunduki' hao.

"Tulikuwa vizuri sana kwa kwenda mbele na tulikuwa na nguvu nzuri ya kufanya hivyo," alisema Arteta.

"Tulifunga mabao matatu mazuri sana, lakini hatukuwa na nguvu nzuri zaidi kwenye ulinzi. Wakati linapotokea, unaweza kuumia."

3,643,920

# JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 12/03/22 | 18:00 | Millwall vs Middlesbrough | 2.22 | 3.20 | 3.15 |
| 02. 12/03/22 | 18:00 | Coventry vs Sheffield Utd | 2.60 | 3.14 | 2.65 |
| 03. 12/03/22 | 18:00 | Blackpool vs Swansea | 2.36 | 3.29 | 2.85 |
| 04. 12/03/22 | 19:00 | Montpellier vs Nice | 3.02 | 3.47 | 2.24 |
| 05. 12/03/22 | 23:00 | Troyes vs Nantes | 2.63 | 3.22 | 2.68 |
| 06. 12/03/22 | 23:00 | Getafe vs Valencia | 2.46 | 3.06 | 3.06 |
| 07. 12/03/22 | 23:30 | Belenenses vs Boavista | 2.71 | 3.25 | 2.51 |
| 08. 13/03/22 | 14:15 | Fortuna Sittard vs Willem II Tilburg | 2.80 | 3.35 | 2.48 |
| 09. 13/03/22 | 15:00 | Luton Town vs QPR | 2.25 | 3.20 | 3.10 |
| 10. 13/03/22 | 15:30 | Hannover vs Nurnberg | 2.50 | 3.24 | 2.70 |
| 11. 13/03/22 | 17:00 | Angers vs Reims | 2.27 | 3.13 | 3.28 |
| 12. 13/03/22 | 17:00 | Strasbourg vs Monaco | 2.37 | 3.32 | 2.92 |
| 13. 13/03/22 | 17:00 | Everton vs Wolverhampton | 2.29 | 3.26 | 3.16 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMANNE - 08/03/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 3254 | Gaddafi FC vs Express FC | 5.79 | 3.52 | 1.55 |
| 15:40 | 4069 | Hajer Club vs AL Sahel SC | 2.30 | 2.78 | 3.26 |
| 16:00 | 1840 | AL Akhdood vs AL Jeel | 2.17 | 3.10 | 3.60 |
| 16:00 | 5524 | Enppi Club vs Eastern Company SC | 1.30 | 5.11 | 9.24 |
| 16:15 | 2896 | Bisha FC vs AL Kawkab | 2.80 | 2.85 | 2.56 |
| 17:00 | 3805 | Churchill Brothers vs Sudeva Delhi FC | 1.55 | 3.69 | 5.37 |
| 18:00 | 1201 | Mladost Lucani vs FK Vozdovac | 2.08 | 3.14 | 3.33 |
| 18:00 | 5239 | FC Krasnodar II vs Baltika Kaliningrad | 8.07 | 4.51 | 1.33 |
| 18:15 | 5282 | Al Sadd SC vs Al Rayyan SC | 1.15 | 7.12 | 11.55 |
| 18:30 | 5446 | Ceramica Cleopatra vs Smouha Club | 3.16 | 2.92 | 2.40 |
| 20:00 | 2719 | Hermanstadt vs Universitatea Cluj | 2.36 | 3.13 | 2.80 |
| 21:00 | 2037 | Al Ahly Cairo vs Pyramids | 1.78 | 3.35 | 4.63 |
| 22:30 | 3872 | Wimborne Town vs Yate Town | 5.78 | 4.34 | 1.44 |
| 22:30 | 5712 | Stenhousemuir vs Kelty Hearts FC | 4.25 | 3.62 | 1.70 |
| 22:45 | 1032 | Southend vs Grimsby | 2.78 | 3.27 | 2.38 |
| 22:45 | 1686 | Maidenhead U vs Wealdstone | 2.04 | 3.51 | 3.22 |
| 22:45 | 1695 | Barnsley vs Stoke City | 2.90 | 3.19 | 2.37 |
| 22:45 | 2128 | Blackburn vs Millwall | 2.12 | 3.09 | 3.53 |
| 22:45 | 2226 | Kings Lynn vs Woking | 3.42 | 3.56 | 1.95 |
| 22:45 | 2352 | Warrenpoint vs Dungannon Swifts | 2.32 | 3.51 | 2.60 |
| 22:45 | 2380 | Stirling vs Cowdenbeath | 1.74 | 3.61 | 4.05 |
| 22:45 | 2383 | Yeovil vs Dagenham and Redbridge | 2.41 | 3.37 | 2.68 |
| 22:45 | 2506 | Wrexham vs Boreham Wood | 1.70 | 3.66 | 4.49 |
| 22:45 | 2543 | Altrincham vs Weymouth | 1.94 | 3.61 | 3.41 |
| 22:45 | 2663 | Potters Bar Town vs AFC Hornchurch | 4.13 | 3.80 | 1.68 |
| 22:45 | 2729 | Bournemouth vs Peterborough | 1.27 | 5.28 | 9.59 |
| 22:45 | 2763 | Wigan vs Sutton United | 1.53 | 3.96 | 5.21 |
| 22:45 | 2957 | Crusaders Belfast vs Coleraine FC | 2.00 | 3.13 | 3.56 |
| 22:45 | 3308 | Solihull Moors vs Notts County | 2.35 | 3.32 | 2.78 |
| 22:45 | 3358 | Ballymena Utd vs Linfield Belfast | 4.13 | 3.70 | 1.70 |
| 22:45 | 3563 | Taunton Town vs Merthyr Town | 1.20 | 6.18 | 9.66 |
| 22:45 | 3633 | Larne vs Glenavon | 1.59 | 3.85 | 4.72 |
| 22:45 | 4027 | Morpeth Town vs Warrington Town | 2.34 | 3.75 | 2.70 |
| 22:45 | 4301 | Crewe vs Portsmouth | 4.11 | 3.48 | 1.82 |
| 22:45 | 4346 | MK Dons vs Cheltenham | 1.72 | 3.68 | 4.42 |
| 22:45 | 4353 | Glentoran Belfast vs Cliftonville Belfast | 1.71 | 3.75 | 4.03 |
| 22:45 | 4901 | Swansea vs Fulham | 4.30 | 3.62 | 1.75 |
| 22:45 | 5085 | Ipswich vs Lincoln | 1.68 | 3.73 | 4.62 |
| 22:45 | 5185 | Merstham vs Cheshunt | 3.81 | 3.66 | 1.77 |
| 22:45 | 5224 | Coventry vs Luton Town | 2.13 | 3.14 | 3.43 |
| 22:45 | 5382 | Sheffield Utd vs Middlesbrough | 2.04 | 3.29 | 3.49 |
| 22:45 | 5463 | Partick Thisle vs Queen of South | 1.42 | 4.30 | 6.84 |
| 22:45 | 5514 | Exeter vs Swindon Town | 2.09 | 3.43 | 3.23 |
| 22:45 | 5665 | Carrick Rangers vs Portadown FC | 1.97 | 3.33 | 3.43 |
| 22:45 | 5673 | Sunderland vs Fleetwood Town | 1.52 | 4.13 | 5.51 |
| 22:45 | 5828 | Plymouth vs AFC Wimbledon | 1.76 | 3.58 | 4.32 |
| 23:00 | 1148 | Bayern Munchen vs RB Salzburg | 1.19 | 7.39 | 11.99 |
| 23:00 | 1279 | Liverpool vs Inter | 1.57 | 4.31 | 5.21 |
| 23:00 | 2614 | Bolton vs Morecambe | 1.54 | 4.14 | 5.32 |
| 23:15 | 3530 | Casa Pia Atletico vs Mafra | 1.86 | 3.36 | 4.00 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.




# SAMATTA KUICHANGIA TWIGA STARS

**Na Saada Akida**

NAHODHA wa Timu ya Taifa ya Soka ya Tanzania, Mbwana Samatta na mamia ya watu maarufu wamejitokeza kuchangia timu ya Taifa ya Wanawake ya Twiga Stars katika kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani kupitia Tamasha la The Orange Concert leo Machi 8, jijini Dar es Salaam.

Akizungumzia kuhusu tamasha hilo, Sammata amesema anaipongeza serikali kupitia Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa ubunifu wa kuandaa tamasha hilo la kihistoria kwenye Siku ya Wanawake Duniani kuwachangia Twiga Star ili waweze kuendelea kufanya vizuri katika mashindano ya kimataifa.

"Mimi Mbwana Samatta nahodha wa timu ya taifa, natambua kazi kubwa wanayofanya dada zetu wa Twiga Stars katika ramani ya michezo, naungana na serikali yangu nikisema tano kwa Twiga Stars katika tamasha hili la The Orange Concert, " alisema Samata.

Samatta ametoa wito kwa Watanzania wote kuunga mkono jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan za kuendeleza michezo kwa kuwachangia Twiga Star ambapo alisema wanawake wamekuwa wakifanya vizuri, hivyo jamii inawajibu wa kuwasaidia kwa hali na mali ili wafanye vizuri na kuiweka Tanzania kwenye ramani ya kimataifa katika michezo.

# Ajibu, mashabiki bega kwa bega

**Na Shufaa Lyimo**

KIUNGO wa Azam FC, Ibrahim Ajibu, amewataka mashabiki wake kuendelea kumwamini kutokana na ubora wake.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, mchezaji huyo alisema lengo lake kubwa ni kuifikisha mbali timu yake hiyo, hivyo sapoti ya mashabiki ni muhimu ili kutimiza azma yake hiyo.

"Mikakati yangu ni kuifanyia mazuri klabu yangu ili tushike nafasi za juu kwenye msimamo wa Ligi Kuu," alisema Ajibu.

Alisema anashukuru kuona mashabiki wake bado wanamkubali jambo ambalo linampa moyo wa kuzidi kujituma ndani na nje ya uwanja.

"Ninashukuru kusikia mashabiki wangu bado wananikubali, ninaahidi kutowaangusha," alisema.

Akizungumzia mchezo uliopita ambao waliupoteza mbele ya timu ya Polisi Tanzania, alisema kuwa ni moja kati ya matokeo ya mpira, na kuwataka mashabiki waendelee kuwaunga mkono.



# Michezo



Jumanne Machi 8, 2022

Nipashe


De Gea: Tutairejesha Man U inapostahili UKURASA 21

TUTANGAZENI...



Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro (kushoto) na Balozi wa Tanzania nchini Uholanzi, Irene Kasyanju (watatu kushoto), pamoja na watumishi wa Ubalozi wa Tanzania nchini humo wakitembezwa Uwanja wa Klabu ya Ajax na Meneja Masoko wa klabu hiyo, Ted Robinson (wapili kushoto), baada ya kuutembelea kwa ajili ya kufanya mazungumzo ya kuiomba kutangaza vivutio vya utalii vya Tanzania kupitia jezi na mabango ya matangazo uwanjani hapo. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Nabi alia majeruhi, ageukia waamuzi

## ●●● Awataka kulinda wachezaji na kuacha kumezea rafu mbaya kwa kutotoa kadi, huku akitaja...

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, ameonyesha kufurahishwa na ushindi wa bao 1-0 walioupata dhidi ya Geita Gold FC juzi kwenye Uwanja wa CCM Kirumba, jijini Mwanza, lakini akaonyesha kusikitishwa na kuwapo kwa rundo la majeruhi kwenye kikosi chake, huku akiwataka waamuzi wanaochezesha Ligi Kuu kulinda wachezaji na rafu za makusudi zinazofanywa.

**Wakati Nabi akisema hayo, Kocha Mkuu wa Geita Gold, Fred Felix Minziro, alisema ni umakini wa wachezaji wake ndiyo uliowanyima ushindi, kwani waliikamata Yanga kipindi cha pili na kuutawala mchezo huo.**

Hata hivyo, Nabi alisema kuwa walilazimika kujilinda kipindi cha pili ili wasiruhusu bao kutokana na ubora walioonyesha Geita Gold kwenye mechi hiyo.

"Tulifunga goli la mapema ambalo liliwafanya Geita kuanza kutushambulia, nikaamua kuipanga timu yangu icheze kwa kulinda ushindi ili kupata alama tatu muhimu," alisema kocha huyo na kuongeza.

"Lengo langu ni timu icheze mpira na tupate ushindi, si kujilinda. Geita wamepata matokeo na hawajapoteza katika mechi zao zote nne zilizopita, tuliwaheshimu lakini si kwamba wametuzidi, ila tuna majeruhi wengi na imefika wakati wa kucheza kimbinu kusaka ushindi," alisema Nabi.

Kocha huyo alisema idadi kubwa ya wachezaji wao ni majeruhi na hii inatokana na mara nyingi wakati wa kugongana na wachezaji wa timu pinzani.

"Tunajua kuwa ligi ni ngumu na kila timu inahitaji pointi tatu, lakini waamuzi wanatakiwa wawalinde wachezaji na si kwa Yanga tu, bali hata wa timu nyingine ili timu isizalishe majeruhi wengi bila sababu.

"Kuna mchezaji wa Geita Gold alimpiga kiwiko Bakari Mwamnyeto, lakini mwamuzi aliacha tu, siyo kwamba hakuona, muda mfupi baadaye mchezaji huyo huyo akamkanyaga Dickson Job na rafu zote hizo zilikuwa ni za kadi nyekundu," alisema kocha huyo huku akikumbushia mechi iliyopita ambayo Saido Ntibazonkiza naye alichezewa rafu ya makusudi.

Kwa upande wa Minziro alisema kuwa umakini ullikosekana kwa wachezaji wake, kwani zilipatikana nafasi tatu mpaka nne za kuimaliza mechi hiyo.

"Mmeona wenyewe mechi hiyo na kila mtu ameiona, walipata bao la mapema na angalau kipindi cha kwanza walifanya mashambulizi ya maana, kipindi cha pili tuliwabana na hawakufanya shambulizi lolote la maana. Ni sisi wenyewe tu kutokuwa makini," alisema Minziro.

# Pablo na ugumu ratiba Simba SC

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI jana usiku akikiongoza kikosi chake kuikaribisha Dodoma Jiji FC kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Kocha Mkuu wa Simba, Pablo Franco, amelia na ugumu wa ratiba huku akieleza ni moja ya chanzo kikubwa cha kuelemewa na majeruhi wengi kikosini.

Simba jana iliivaa Dodoma Jiji ikiwa ni siku tatu tangu icheze dhidi ya Biashara United, lakini mechi zake nyingi imekuwa ikicheza kila baada ya siku tatu hadi nne, huku ikikabiliwa na ratiba ngumu ya mechi za kimataifa, Kombe la Shirikisho Afrika.

Akizungumza na mwandishi wetu, Pablo alisema ratiba imekuwa ngumu kwao na hawapati muda wa kujiandaa kutoka mechi moja hadi nyingine, lakini hawana budi kuhakikisha wanapambana katika kila mchezo ili kupata alama zote tatu.

"Kwa ujumla ratiba imekuwa ngumu, uwiano wa mechi moja hadi nyingine ni mdogo, hatuna muda wa kutosha kufanya mazoezi ya utimamu wa mwili, na hii imekuwa ikichangia kuwa na majeruhi wengi," alisema kocha huyo raia wa Hispania.

Baada ya mechi hiyo ya jana, Simba itashuka tena dimbani hapo Jumapili wiki hii kuikaribisha RS Berkane ya Morocco kwenye Kombe la Shirikisho Afrika kabla ya kukwea pipa kwenda kuivaa Asec Mimosas Machi 20, mwaka huu na kisha wiki moja baadaye kutua Mbeya kuvaana na Tanzania Prisons.

Kabla ya mchezo huo wa jana, Simba ilikuwa nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara ikiwa pointi 11 nyuma ya vinara Yanga wenye alama 45, lakini wakiwa mchezo mmoja mbele, na kwa upande wa Kombe la Shirikisho Afrika, wawakilishi hao pekee wa Tanzania kimataifa, wana alama nne sawa na USGN ya Niger, zikiwa nyuma ya vinara RS Berkane yenye pointi sita, huku Asec Mimosas wakiburuza mkia kwa pointi zao tatu.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >